Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 79 No. 199 | RAB. I - RAB. II 1439 AH | DISEMBA 2018 | FATAH 1397 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Wamewafanya wanazuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu na Masihi mwana wa Mariamu pia; hali hawakuamrishwa isipokuwa kumwabudu Mungu Mmoja, hakuna aabudiwaye ila Yeye, Ametakasika na yale wanayomshirikisha nayo. (9:31)

Sifa za Waahmadiyya wa Kweli

Na Mwandishi Wetu

Katika hotuba ya tarehe 26/10/2018 Baada ya Tashahhud,Taawwudh na Surat Faatihah, Hadhrat Amir-ul Muminiin[atba] alisema:

Hii ni hisani kubwa ya Allah Subhanahu wataala juu yetu ambaye kwa fadhila Zake Alituwezesha kumpokea Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa[as] na Aliyetujaalia kumkubali yule mtumishi mkweli ya Mtume Muhammad[saw] aliyetajwa naye kuwa "Mahdi Wetu". Hiki ni cheo cha hali ya juu kabisa cha upendo na ukaribu kilichodhihirishwa na Mtume Muhammad[saw] alivyomtaja Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa[as] kwa maneno ya "Mahdi Wetu". Pale Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa[as] alipoeleza katika vitabu vyake kwamba dini tukufu ya kiislam ni bora kuliko dini zingine zote na kwa kuzirudisha kwao shutuma za wapinzani akathibitisha kwamba leo hii kama dini yoyote inapatikana duniani iliyo sahihi na inayoweza kuleta ukaribu na Allah Subhanahu wataala na kuokoa na madhambi, basi ni dini tukufu ya kiislam pekee. Vile vile aliweza kutoa nasaha nyingi katika hotuba na maandiko na vikao vingine na watu kwa ajili ya malezi ya wafuasi wake ambazo ni mwongozo kwetu



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akitoa hotuba ya Ijumaa kwa wanajumuiya katika msikiti mpya uliofunguliwa huko Philadelphia iliyopo Amerika ya kati.

katika kila hatua ya maisha yetu. Yeye aliwasisitizia kwa uchungu wafuasi wake kutimiza haki za Bai'at na kuwa waaminio wakweli. Tunatakiwa tuzizingatie nasaha hizi kikamilifu. Na hii ndio njia ya malezi yetu ya kiroho. Tunaweza kuifahamu ipasavyo elimu ya dini kwa kupitia njia hii tu. Na hii ndio njia inayotuwezesha kutafuta njia nyingine za kuupata ukaribu na Allah Subhanahu wataala. Hii ndio njia ya kufikia maana ya kina ya Quran tukufu. Na hii ndio njia ya kuelewa vizuri cheo cha ubora wa Mtume Muhammad[saw]. Na hii ndio njia inayotuwezesha kurekibisha hali zetu za kiitikadi. Na hii ndio njia pekee inayotusaidia kuboresha hali zetu za kimatendo. Hii itakuwa bahati mbaya kama tusiponufaika na hazina hii. Athari ya kiroho inayopatikana katika maneno ya Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa[as] haiwezi kupatikana katika maneno ya mtu mwingine yeyote. Na kwa nini isiwe hivyo? Yeye ndiye Imamu aliyemtuma Allah subhana wataala kuwa mtumishi wa Mtume Muhammad[saw] katika zama hizi ili kuhuisha Islam mara ya pili na kuupata ukaribu na Allah Subhana wataala. Huu ni wajibu wetu sisi ambao tunakiri kuungana na Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa[as] kwamba tusome maneno yake, kuyaskiliza na kuyatekeleza. Tunatakiwa kujiboresha hali zetu jinsi tulivyotarajiwa na Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa[as].

Sasa ningependa kuweka mbele yenu baadhi ya nasaha za Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa[as] ambazo ni mtaala wa maisha yetu na shabaha aliyoweka mbele yetu na kueleza kila mwahmadiyya anatakiwa kuwa na kiwango gani. Katika dunia hii yenye vishawishi vingi vya kimwili umuhimu wa mambo haya umeongezeka sana. Hususan wakati ambapo baadhi yetu huelekea zaidi kwenye dunia na dini hawaiheshimu ipasavyo. Sisi

Endelea uk 4

Krismasi na Yesu Kristo Hakuna Uhusiano

Maktaba Yetu

Ukizunguka katika maduka makubwa wakati wa Msimu wa Sikukuu ya Krismasi kwa hakika ni lazima ukutane na wimbo maarufu wa '*I am Dreaming of the White Christmas*' ukihanikiza eneo hilo kwa mbaali. Kwa kadri hali ya joto inavyozidi kupungua, kwenye baadhi ya maeneo yenye baridi kali, watu huipamba sikukuu ya hii ya Krismasi kwa kuuvaa uhusika wa Santa na mavazi yake. Lakini, Santa si tu hupatikana kwenye maeneo yenye hali ya baridi kali, bali pia huonekana kwenye maeneo ya fukwe zenye starehe nyingi kule Australia kila ifikapo Disemba 25.

Msimu wa Krismasi pia huwa ni muda muafaka katika ulimwengu wa burudani ambapo filamu mbalimbali huoneshwa kuhusu asili ya Krismas, Santa, maigizo na drama za watoto. Katika shamrashamra za Krismasi, muda huu pia huwa ni mahangaiko yote ya maandalizi ya Krismasi, mahususi kwa watu kutoa misaada mbalimbali kwa watu wasio na makazi na wale walio masikini hohe hahe.



Wasomi na Wanazuoni wengi wa Kikristo wanamtazamo kuwa Nabii Issa au Yesu[as] kama anavyotajwa na waumini wa dini ya Kikristo kuwa hakuzaliwa tarehe 25 Disemba kama inavyoaminiwa na mamilioni ya Wakristo duniani kote. Mtakatifu Papa Benedict XVI pia anaiunga mkono hoja hiyo.

Utoaji wa misaada ni jambo mahususi ambalo hufanya watu nje ya sikukuu hii kwa watu kutoa zawadi, vyakula namalazi kwa masikini ambapo jambo hili huenea sehemu kubwa ulimwenguni ambapo hata katika nchi masikini taratibu mbalimbali hufanywa kwa lengo la kuwafariji watu masikini wa kutupwa. Sikukuu ya Krismasi huenda mbali kwa kuwaunganisha ndugu na marafiki, ikibidi hata kwa watu kusafiri kutoka upande mmoja wa dunia kwenda upande mwingine kuungana na familia na wapendwa wao. Bila kujali hali yeyote ya uhasama au kutoelewana baina ya ndugu, nyota njema ya Sikukuu ya Krismasi huwaunganisha wapendwa na kuwawezesha kujumuika

Endelea uk 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

KITABU KWA SIKU

Neno lolote linalotolewa na Nabii wa Allah, sisi waja kwaheshima na taadhima tunatakiwa tukae kitako na kutafakari juu ya neon hilo. Ni ukweli wa kwamba, manabii wa Allah hupewa buruhani na muumbaji wa mbingu na ardhi na hivyo maneno yao yakawa na hekima na busara kubwa.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa aliwahi kutoa kauli ambayo ina ujumbe mzito na unaotakiwa kufanyiwa kazi. Alisema wakati wangu hautapotezwa. Nani kwa hivi leo asiye maize umuhimu mkubwa wa rasilimali hii iitwayo wakati. Kuna misemo mingi katika lugha nyingi ikisisitiza juu ya umuhimu wa kuheshimu wakati. Lugha ya kiingereza ina msemo usemao wakati ni mali. Na moja ya kebehi kubwa kwa bara la Afrika ni kwamba hatuna wasiwasi na wakati kwani wakati upo tu. Kwa vyoyote vile fikra ya namna hii ni potofu na haiwezi kuiletea jamii yeyote maendeleo. Mwandishi maarufu wa kiingereza William Shakespear anasema "nilipoteza wakati na sasa wakati unanipoteza mimi".

Wanaoidharau Afrika wanapenda sana kutumia mfano wa nchi ya Sudan wakitolea mfano juu ya shirika lao la ndege ambalo limepewa jina la InshAllah.

Ukienda saa mbili wakati mlipoahidiwa kwamba mnaondoka watakuambia InshAllah saa tatu na ikifika saa tatu wanakuambiaInshAlla saa nne. Basi siku nzima inatawaliwa na utamaduni huo wa InshAllah. Ikiumbukwe ya kwamba hii siyo maana sahihi ya neno InshAllah bali ni visingizio vya kutoheshimu wakati. Sudani ikiwa nchi ya Kiislamu wanaelewa utaratibu wa sala na wakati.

Kwa msikitiko makubwa katika ofisi nyingi hakuna kinachofanyika isipokuwa wingi wa soga za Manchester na Arsenal na Simba na Yanga ilimuradi katika maradhi yanayolisibu Taifa letu ni mwenendo huo wa kupoteza wakati. Hili ni jambo ambalo tunatakiwa kutafakari.

Kuelewa tatizo ni rahisi. La msingi ni kutafuta dawa mjarabati wa kutatua tatizo hilo. Fikiria mtu ameamua kwenda Bagamoyo ili kuongeza elimu yake juu historia yetu. Kapanda gari kiwalani kufika Buguruni kuna msururu wa magari umeshonana mnakwenda taratibu kana kwamba mnasindikiza bi harusi. Unapiga miayo wakati unapotea. Ungekumbuka kubeba kitabu yasingekukuta yote hayo. Kwa nini ukubali kutoka nyumbani kwako bila ya kitabu kwenye mkoba? Ni njia nzuri ya kutumia vizuri wakati. Bado mpaka hivi leo tunao maofisa ambao furaha yao wakiona msururu wa watu wakiwasubiri ili wawaone. Utakaa muda mrefu ukifyonya na kupiga miayo ebu fikiri kama ungebeba kitabu. Hapana shaka ungekuwa na rafiki wa kuzungumza nae. Tunapoteza wakati mwingi bila ya kubeba kitabu mkononi. Kwa nini tusijenge utamaduni huu wa kubeba kitabu? Kwa nni tusipitishe azimio kuwa sasa kwamba hatutapoteza wakati tena. Hapana shaka kuwa hili linaweza kuwa azimio bora wakati tunaingia mwaka wa 2019 InshAllah. Gazeti la Mapenzi Ya Mungu linawatakia baraka na fanaka ya mwaka 2019.

Krismasi na Yesu Kristo Hakuna Mahusiano

Kutoka uk. 1

pamoja wakati huo huo wakifurahi chakula mahususi cha Krismasi.

Bila kujali ikiwa watu wanajua nini hasa maana ya kweli ya Krismasi au la, sikukuu hii hutoa nafasi ya watu kutoa na kushirikiana. Kwa hakika kuna mengi mazuri yanayofanywa wakati wa Krismasi; ingawaje ukitafakari, unajiuliza Krismasi inahusu nini?

Jambo la kwanza watu kuhusishwa na Krismasi ni kuzaliwa kwa Yesu[as]. Ingawa, mada kuhusu kuhusu tarehe hasa ya kuzaliwa kwa Yesu[as]



Qur'ani Tukufu inaelezea kuzaliwa kimiujiza kwa Yesu[as] na kusema kwamba, kwa mpango maalumu wa kimbingu, Maryam, Mama yake Yesu[as] , alifikia chini ya mti wa tende zilizoiva, kuelezea kwamba kipindi cha kuzaliwa kwa Yesu[as] kilikuwa ni msimu wa kiangazi, kuliko Disemba kama wengi wanavyoamini.

imekuwa ikijadiliwa kwa miongo kadhaa sasa. Wanazuoni na Wanatheolojia wa Kikristo akiwemo Mtakatifu Papa Benedicto XVI , anakubali kuwa Yesu[as] hakuzaliwa Disemba 25. Kiasili, mtu anaweza kuyageukia maandiko kama chombo chenye mamlaka ya kuamua ukweli hasa wa tatizo tunalokumbana nalo ni kwamba hakuna pahala popote panapoonesha kuwa Yesu[as] alizaliwa Disemba 25 au tarehe nyingine yeyote katika Agano Jipya. Tunachoweza kukiona katika Agano Jipya ni alama tu za lini inaweza tukio la kuzaliwa kwa Yesu[as] kilitokea; Injili ya Luka inatoa mwanga kuhusu jambo hilo kwa kusema:

Na katika nchi ile ile walikuwako wachungaji wakikaa makondeni na kulinda kundi lao kwa zamu usiku.

Kulingana na mlango huo wa Biblia, wachungaji walikuwa wakiwatazama kondoo wakati wa kuzaliwa kwa Yesu[as]. Ni jambo lisilokubalika kwamba wachungaji wawe wakiwatazama kondoo wao katika usiku wenye baridi kali wa kipupwe cha mwezi Disemba, hii inamaanisha kwamba kipindi cha malisho ya kondoo kilikuwa ni kipindi cha majira ya joto, si mwezi Disemba. Kuhusiana na hili, Albert Barnes, mwanazuoni na mwanatheolojia wa Kimarekani wa karne ya 14 anaadika katika maelezo yake;

'Inakadiriwa ya kwamba mwokozi wetu alizaliwa kabla ya 25 Disemba, au kabla ya tunachokiita 'Krismasi'. Nyakati hizo ni baridi, na hususan kwenye miinuko na maeneo ya milima karibu na Bethlehem. Lakini muda hasa wa kuzaliwa kwake haujulikani; hakuna njia ya kuuhakikisha.'

Watoa maoni wengine wa Biblia wanakisia kwamba kuzaliwa kwa Yesu[as] kulitokea katika msimu wa joto. Qur'an Tukufu pia inatoa mwanga katika hili:

'Mara ikamfikia sauti kutoka chini yake: Usihuzunike, hakika Mola wako Ameweka kijito chini yako; Na ulitikise kwako shina la mtende, litakuangushia tende nzuri, zilizo mbivu. Basi ule na unywe na uburudishe macho;' (19: 25-27)

Hizi aya kuhusu kuzaliwa kwa Yesu[as] zinaeleza namna Mariam alivyojipatia kivuli chini ya mtende kipindi cha kujifungua na Mungu alimruzuku tende akala; hivyo hili lisingewezekana Disemba, wakati tende hazijaiva.

Swali huzuka, je, kama Disemba 25 si tarehe ya kuzaliwa Yesu[as] basi namna gani na lini sherehe za Krismas na mila zake ziliingia kwenye himaya ya Ukristo?

Ushahidi wa kihistoria unatuambia kwamba *'sababu ya Krismasi ikasherehekewa Disemba 25 bado hazina uhakika, lakini sababu inayokisiwa zaidi ni kwamba Wakristo wa mwanzoni walitamania tarehe iwiane na ya Wapagani Warumi wakiadhimisha "kuzaliwa kwa mungu jua" (**natalis solis invicti**); sherehe hizi zilifanyika msimu wa baridi, ambapo siku huwa ndefu na jua huanza kuwa mbali angani'.*

Kama mtafiti David Ingraham anavyoandika, ***'Mnamo 375 A.D, Kanisa lilitangaza kwamba tarehe ya kuzaliwa kristo imegundulika kuwa ni Disemba 25. Hii tarehe haikuwa na misingi ya kihistoria au Kibiblia, hata hivyo na ikawa rasmi kwa ajili ya upatanisho ili sherehe za kuzaliwa Kristo ziungane na sikukuu za msimu wa mapagani.'***

Sikukuu ya Krismasi ilisimilishwa kiwepesi na kanisa kutumia mchakato wa syncretism kwa ajili tu ya malengo yao kuidaia kama siku ya kuzaliwa Yesu[as] na kuisherehekea vilivyo. Ensaiklopidia Mpya ya Katoliki inasema,

'Krismasi ilianzia wakati ambapo dini ya jua ilikuwa imara haswa Roma. Nadharia hii inapata nguvu katika

Endelea uk. 3

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Sheikh Abdulrahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Krismasi na Yesu Kristo Hakuna Uhusiano

Kutoka uk. 2

baadhi ya Wazee wa kanisa wakiainisha kuzaliwa kwa Kristo na msimu wa baridi. Ingawa mbadilishano wa Krismasi kwa sikukuu za kipagani haziwezi kuhakikishwa, unabakia kuwa kitendawili kikubwa kisichojibiwa uupaji tarehe wa Krismasi.'



Mnamo 375 CE Wakuu wa Kanisa walitamka 25 Disemba kuwa siku rasmi ya kuzaliwa Yesu[as]. Inaonekana kuwa ilikusudiwa kupatanishwa na sikukuu ya Wapagani ya jua iitwayo Natalis Solis Invicti.

Krismasi ilianzia Roma na tarehe ya kuzaliwa kwa Yesu[as] na mila za Saturnalia na sikukuu za Yule zilizojibadili kiustadi na taratibu kutapakaa ulimwenguni. Mila aina zote maarufu za Krismasi kama vile mti wa Krismasi, miti ya mistletoe kutoa zawadi na Baba Krismasi (Santa) zote zina msingi wa kihistoria katika mila za kipagani.

Watu wengi huiona Krismasi kama sikukuu ya kidini ambapo familia hukutana na kusherehekea pamoja, lakini hakuna maungano ya kweli kati ya Krismasi na Yesu[as] kabisa. Krismasi, kuwa kwake imeasisiwa kwa karne nyingi, ni maarufu mno, yenye kufurahisha na ni tamaduni yenye mizizi iliyokita kwa watu kiasi kwamba inakuwa ngumu kwao kuitelekeza au kuacha kuisherehekea.

Hata hadithi ya Santa (Baba Krismasi) imekuwa ikijadiliwa, hususan juu ya kuwadanganya watoto kuhusu Santa kuna madhara au la. Akiandika katika *The Lancet Psychiatry*, mwanasaikolojia Christopher Boyle na mtafiri Kathy McKay wanaeleza kwamba hadithi hiyo inapelekea kutoaminiwa: ***'Kama wanadiriki kudanganya juu ya kitu maalum na cha maajabu, wanawezaje kutegemewa juu ya kuendelea kuwa walinzi wa ukweli na busara?'***



Licha ya fumbo linalozunguka kuzaliwa kwa Yesu[as], kazi yake ilikuwa wazi; kuwakusanya makabila yaliyopotea yaliyopelekwa uhamishoni kutoka Yerusalem, kwanza na Wasiria na kisha na Babilonia. Kama Masihi Aliyeahidiwa[as] alivyodhihirisha, walisafiri kupitia njia ya kibiashara, baadhi wakakaa Afghanistan na wengine Kashmir.

Wakati kuna utofauti wa maoni ya wazazi inapokuja kwenye kuwaelezea watoto asili ya Krismasi, sehemu kubwa ya wazazi huenda wasitilie vitu fulani maanani. Jambo hasa ni kwamba kama kila kitu kuhusu Krismasi ikiwemo tarehe ya kuzaliwa kwake Yesu[as] haiko barabara basi watoto huenda wakakua na shaka juu ya imani yao, wakijiuliza ukweli hasa ni upi. Kutoka kwenye mtazamo wa kidini hii inawezekana kuonekana kama mtihani mgumu wa kiimani huswa kwa sababu sherehe kama ya Krismasi haiwiani na maelezo ya Biblia na haiwezi kutambulika kama uhalisia.

Licha ya umaarufu wa sherehe za Krismasi katika Disemba 25, tatizo ni kwamba hakuna ushahidi wa kiteolojia (elimu ya dini) katika nyaraka zozote za zamani za Biblia au maandishi ya kuunga mkono maungano yake na Yesu[as]. Yesu[as] hakufanya Krismasi wala hakufundisha wengineo kuifanya. Yesu[as] kwa hakika alizaliwa kwa mama yake mtawa Mariam uzao wa maajabu wa kibikira na akaja duniani kwa shabaha maalum. Tukiakisi kwenye shabaha ya Yesu[as] kuja duniani na jukumu lake, tunajifunza kutoka Agano Jipya kwamba Yesu[as] alikuwa mfuasi wa dhati wa Agano la Kale ambalo lilifundisha dhidi ya ibada ya masanamu, kwa hiyo katu haiyumkiniki kwa Yesu[as] kuwa angewataka wafuasi wake wamuabudu kama sanamu baada ya kifo chake.

'Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza.'

Hii aya katika Injili ya Mathayo inatuambia namna ambavyo Yesu[as] alikuwa mfuasi mwaminifu wa sheria ya Agano la Kale, ambayo ilionya juu ya kuzifuata mila za kipagani kumuenzi.

Usherehekeaji wa Krismasi katika baadhi ya sehemu za dunia kama vile uandaaji dhifa au sherehe na kujiingiza katika vitendo vya kukithiri kwa hakika si ambavyo Yesu[as] angewaelekeza wafuasi wake kufanya. Krismasi imekuwa ikiendelea kusherehekewa bila ya kujiuliza kuhusu asili yake haswa au maana yake ya kweli.

Hata hivyo, kuna vitu vizuri vinavyotokea katika msimu wa sikukuu hizi katika nchi nyingi kama vile juhudi za kuwalisha na kuwaangalia watu wa mitaani na vitendo vingi vya wema, ambavyo Yesu[as] alivifundisha kwa upole.

Msimu wa sikukuu hii ni muda mzuri kutafakari shabaha ya kweli na maisha ya Yesu[as] na kazi yake duniani ya kuwaongoza watu kufuata sheria ya Musa, na kuwakusanya kondoo waliopotea wa Izraeli. Wakati huo huo Yesu[as] pia aliwaongoza watu kuhusu tabiri za baadae hususan kuhusiana na ujio wake wa mara ya pili.

Kama wafuasi wa Masihi wa kweli Aliyeahidiwa[as], tunaona kwamba hatuna budi kuueneza ujumbe kwamba Masihi Aliyeahidiwa[as] ameshafika.

Masihi Aliyeahidiwa[as] anasema:

'Nawambieni kweli ya kwamba wale waliofufuliwa na Masihias (Yesu) wamekufa, lakini yule ambaye atakunywa kikombe ambacho nimeteremshiwa mimi hatokufa kamwe. Ikiwa kuna mwingine yeyote anayeweza kunena maneno yenye kutoa uzima ninayoyasema na kubainisha hekima kama nifanyavyo, basi mna hiyari ya kusadiki kwamba sitoki kwa Mwenyezi Mungu. Hivyo, kama hekima na weledi huu – ambao hutumika kama maji ya uzima kwa nyoyo zile zilizokufa – haupatikani kwenye chanzo kingine chochote, basi hamna tena udhuru kwa kosa la kuikataa chemchem iliyoteremshwa toka mbinguni. Hakuna mtu duniani awezaye kuizuia.'

VIPINDI VYA KISWAHILI MTA AFRICA

SIKU	WAKATI	WAKATI	WAKATI
Jumanne	12:30 Asubuhi	8:30 Mchana	1:00 Jioni
Alhamisi	12:30 Asubuhi	8:30 Mchana	1:00 Jioni
Jumamosi	12:30 Asubuhi	8:30 Mchana	1:00 Jioni

TANGAZO LA USAILI

Jamia Ahmadiyya Tanzania inawataarifu wanajumuiya wote kuwa kutakuwa na usaili kwa ajili ya wanafunzi wapya kwa mwaka 2019 utakaofanyika tarehe 5 Januari 2019 hivyo wanafunzi wafike Jamia Ahmadiyya Morogoro tarehe 3 Januari 2019 wakiwa na barua za utambulisho kutoka kwa Wabashiri au Maraisi au Waalimu husika.

Wabashiri, Maraisi na Waalimu wanaombwa kuwashauri wanafunzi wenye sifa za elimu ya kidato cha nne kuja kwenye usaili huo ili waweze kutafuta fursa ya kuitumikia Jamaat.

Nawashukuru kwa ushirikiano mzuri,

Mkuu wa Chuo
Jamia Ahmadiyya Tanzania

Sifa za Waahmadiyya wa Kweli

Kutoka uk. 1

Waahmadiyya tunajiita waislamu kiitikadi lakini udhaifu mwingi wa kimatendo unaibuka ndani mwetu. Kila mmoja wetu anaweza kujichunguza sawa na nasaha hizi kwamba wapi tulipo na tunakotakiwa kuwa.
Ni nini uchamungu? Kiwango cha Uchamungu ni nini? Wema ni nini na kiwango chake ni nini? Tuna wajibu gani? Akielezea hayo, safari moja Seyidna Ahmad[as] alisema: Allah Amesisitiza mara kwa mara kupata uchamungu wa kweli unaomridhisha: (*Yaa ayyuhalladhiina Amanuu taqullaha*) "Enyi mlioamini mcheni Allah" kisha pia Akasema: (*Inna Allaha maalladhiinattaqaw walladhiina hum muhsinuun*) yaani, Kwa hakika Allah Yu pamoja na wale wanaomcha na wale wafanyao wema (16:129).
Akasema "Uchamungu ni kujiepusha na uovu na Muhsinun ni wale ambao si tu kwamba wanajiepusha na uovu bali wanatenda wema". Akasema tena *lilladhiina Ahsanul husnaa* yaani hutenda mema kwa namna iliyo bora. Alisema "wahyi huu nilifunuliwa mara nyingi mno hadi siwezi kuzihesabu. Allah ndiye Ajuaye sana, huenda nikafunuliwa mara elfu mbili lakini mradi wake ndio huu ya kwamba Jumuiya ifahamu kuwa wasijivunie kujiunga na Jumuiya tu au wasiridhike kupata imani tu. Ukaribu na msaada wa Alllah utapatikana pindi watakapokuwa na uchamungu wa kweli na matendo mema. Si jambo la fahari kwa mtu kuridhika na jambo hili kwamba yeye hazini ama hakumwua yeyote au hakuiba. Huu ni ubora wa namna gani kuwa anaona fahari juu ya kujiepusha na maovu? Hiyo haina umuhimu wowote" yaani kujiepusha kwetu na maovu hakuna umuhimu wowote. "Hakika yeye anajua kwamba akiiba, atafungwa jela kwa mujibu wa sheria. Machoni pa Allah, Islam siyo kujiepusha na maovu tu bali mtu hawezi kupata uhai wa kiroho mpaka ajiepushe na maovu na kushikamana na mema. Mema ni kama chakula na kama vile mtu hawezi kuishi bila chakula, vivyo hivyo bila kutenda mema hana chochote. Basi mkijiepusha na maovu na kushikamana na mema ndipo mtapata uhai wa kiroho. Yapo maovu mengine ambayo yanaathiri maisha ya mtu bila yeye kujua lakini hatimaye ananaswa na mkamato wa Allah kwa sababu ya maovu hayo. Akielezea hayo, Hadhrat Ahmad[as] alisema: "Baadhi ya madhambi ni makubwa kama vile kusema uwongo, kuzini, kuhini, kutoa ushuhuda wa uwongo, kukiuka haki za binadamu na kufanya ushirikina n.k. lakini madhambi mengine ni mepesi ambayo mtu huwa nayo lakini anashindwa kuyatambua. Toka ujanani hadi uzeeni, anashindwa kufahamu kuwa anatenda madhambi, umri wote unapita katika kufanya madhambi bila kujua, kwa mfano tabia ya kutoa malalamiko, kuonyesha huzuni juu ya mambo madogo madogo, kusema maneno kuwa fulani amesema hivi na fulani amesema hivi. Watu wa aina hiyo wanaichukulia kama jambo dogo ilhali Qurani Tukufu imelihesabu kuwa ni kubwa sana. Mambo hayo madogo madogo, kutoa malalamiko, mwishowe yanageuka kuwa kusengenya ndiyo maana Qurani imeihesabu tabia hii kuwa ni jambo kubwa kama isemavyo: (*a' yuhibbu ahadukum an' yakula lahma akhihi maita*). Yaani: Je mmoja wenu anapenda kula nyama ya nduguye aliyekufa? (49:13). Neno la mtu limfedheheshalo nduguye linamchukiza sana Allah. Allah Anasema, je mwapenda kula nyama ya ndugu yenu aliyekufa?
Hazrat Masihi Aliyeahidiwa a.s akasema: Mtu akitamka neno la kumfedhehesha nduguye basi Allah anamkasirikia au mtu akifanya chochote kumletea hasara ndugu yake. Yasiwe maneno tu kwa sababu maneno yanasababisha hasara kwa wengine na yanasababisha malalamiko na watu wanaanza kuwasengenya wengine na kuweka dhana mbaya na mtu hufikia hali ambayo anaanza kumdhuru mtu mwingine. Seyyidna Ahmad a.s anasema: Mtu kusema maneno kuhusu ndugu yake ambayo yanaonyesha ujinga wake au yanasababisha uadui baina yao kisirisiri, mambo hayo yote ni maovu. Vilevile Ubahili na hasira ni vitu vibaya. Basi sawa na amri hii ya Allah, daraja la kwanza ni kuwa mtu ajiepushe na hayo mambo na maovu yote yatokanayo na macho, masikio, mikono na miguu. (mtu asifanye maovu yanayotokana na viungo vyote, na ajitahidi kujiweka mbali na maovu ya aina zote).
Kwa sababu Allah Amesema:
(*Fala takfu maa laisa laka bihii lilmu inna asam'a wa lbasara wa lfu'ada kulu ulaika kana 'anhu masu'la). Yaani wala usifuate usiyo na elimu nayo. Hakika masikio na macho na moyo hivyo vyote vitaulizwa*. (17:37).
(Huzur akaongeza: Baada ya kufa, mtu ataenda kwa Allah na kuulizwa juu ya vitu hivyo).
Seyyidna Ahmad[as] anasema: Maovu mengi yanatokana na dhana mbaya tu. Baada ya kusikia kitu kuhusu mtu fulani, na kukiamini mara moja (bila kufanya utafiti), hiki ni kitu kibaya sana. Kitu ambacho huna uhakika nacho, usikipe sehemu moyoni. Njia hiyo ni kwa ajili ya kuweka mbali dhana mbaya kwamba bila ya kuangalia na kutafakari vizuri, asikiweke moyoni wala asikiongee. Hili ni jambo madhubuti lisilo na shaka ndani yake. Watu wengi watakamatwa kwa sababu ya ndimi zao. (Basi dhana mbaya ikiondoka, nusu ya ufisadi, magomvi na masononeko ya jamii yetu yataisha na umoja utapatikana). Hata duniani, inaonekana kuwa watu wengi wanakamatwa kwa sababu ya ndimi zao na wanafedheheka sana na wanapata hasara. (wanasema kitu na wanakamatwa na ikionekana kama walichosema ni uwongo, hupata aibu kwamba ukweli haujathibitika. Kwahivyo ni bora usiweke dhana mbaya, uweke fikra nzuri kumhusu mwingine, na ukisikia kitu, mwulize kupata elimu. Mwanadamu ni mdhaifu, baadhi ya fikra zinatokea moyoni, ila kama mtu hazitekelezi, Allah Huwa Anasamehe. Allah Haadhibu kwa kuwepo kwa fikra mbaya ila ukizitekeleza ndipo unakamatwa). Kwa kubainisha jinsi gani Allah Anakamata, Seyyidna Ahmad[as] anasema: "Fikra au dhana ambazo hutokea moyoni bila kutekelezwa, mtu hakamatwi. Kwa mfano mtu akipata fikra kuwa apate mali fulani basi itakuwa vyema, hii ni tamaa ya aina moja lakini kama fikra hiyo yenyewe ikija moyoni na kuondoka basi hakuna mkamato. Lakini mtu anapoiweka fikra hiyo moyoni na kupanga njama ya kuipata hiyo mali kwa namna moja au nyingine. (kutafuta mali kwa njia mbaya, kama vile kupata fikra kuwa nimelazimika kulipia kodi kiasi fulani lakini nikitoa kiasi hicho kwa kupunguza kiasi kidogo nitaweza kupata akiba, kupata fikra sio vibaya, Mungu Hakamati ila mtu akiitekeleza, akiiba kodi na kuipatia hasara serikali au hajaongea ukweli katika kuandikisha mapato yake kwa kiasi kidogo katika orodha ya michango, pale Mungu anamkamata. Kuna mifano mbalimbali ya kwamba mapato yao pia yanapungua na kufikia kiasi ambacho waliandikisha kujitolea kifedha katika njia ya Allah na kulipia haki ya serikali.)
Akasema: Dhambi hii mtu atawajibika nayo, kwa hiyo pindi moyo unapodhamiria jambo, ndipo unapofanya ubaya na kuongopa. (Katika watu wa dunia yaani wale wanaopenda dunia sana, baadhi yao ni wafanya biashara na wengineo, wanapokusudia kupata kitu fulani kwa njia isiyo halali linapokuja wazo moyoni wanaanza kupanga mipango na kutekeleza, hivyo amesema dhambi hii mtu atawajibika nayo.) Basi dhambi za aina hii ni mara chache sana watu wanazijali kwa umakini, na hivyo kusababisha maangamio ya mwanadamu. Dhambi kubwa na zile za dhahiri kwa kawaida watu walio wengi hujiepusha nazo. Huenda watu wengi watakuwepo wasiowahi kumwaga damu, wasiomuua mtu, wasionyang'anya, wasioiba, wasiopora wala hawajafanya aina yo yote ya dhambi kubwa, lakini swali ni hili kwamba ni watu wangapi ambao hawajatoa mashtaka ya uwongo kwa wengine dhidi ya mtu, hawajasengenya, hawajafanya dhana mbaya, au hawajamdhalilisha nduguye na kumuumiza moyo? Ni watu wangapi hawajaumiza hisia za ndugu zao au hawajasema uwongo wakiangukia kwenye makosa? (Uwongo nao una aina nyingi, Allah Amewaambia waislamu, yaani yule aliyeamini kwamba usiseme uwongo hata ule ulio mwepesi, mnatakiwa kuwa na ukweli katika kila usemi wenu.)
Amesema: (Ni watu wangapi) Angalau wasiodumu fikra zinazotokea moyoni? Ninaweza kusema kwa yakini kwamba watu wa aina hii watakuwa wachache sana ambao hujali mambo haya.
(Wale ambao hawajamuumiza mtu ye yote, ambao hawajashtaki, hawajafanya dhana mbaya, hawajasema uwongo, na hawajaingiza fikra mbaya moyoni. Watu kama hawa ni wachache ambao wanajali mambo haya na kumuogopa Allah. Hawayafanyi mambo haya kwa sababu tu ya kumuogopa Allah. Yeye anasema badala yake watu wengi ni wale wanaosema uwongo, na katika vikao vyao muda wote wanateta na kuwasengenya wengine. Na wanawafikishia ndugu zao wanyonge na wadhaifu aina kwa aina ya dhiki. Sasa tuangalie vikao vyetu na tufanye tathmini wenyewe, tutaona ya kwamba katika vikao hivyo watu wanazungumziwa vibaya, tunawadhihaki, na kuyaongeza mambo madogo madogo na kwa sababu yake mitafaruku na magomvi yanatokea. Basi hiki ndicho kipimo cha utawa, kinachotegemewa kutoka kwa mwaminio wa kweli.)
Kisha Hazrat Masihi Aliyeahidiwa[as] anasema: Allah anasema kwamba hatua ya kwanza ni kuwa mtu awe mchamungu. Amesema, mimi siwezi kutoa maelezo marefu ya mambo mabaya kwa sasa. Katika Quran tukufu kutoka mwanzo hadi mwisho kuna maelezo ya kina ya maamrisho na makatazo ya Allah. (Yaani ni mambo gani ya kufanya na yepi ya kuyaacha kufanya maelezo yake kamili yanapatikana katika Quran tukufu. Kwa hiyo mwaminio anatakiwa asome Quran kila wakati na aielewe.) Amesema: Quran imeeleza amri za aina nyingi mbalimbali ndani yake. Kwa neno zima ninasema Allah hapendi ufisadi na machafuko katika ardhi, Allah Anataka kueneza umoja duniani. Lakini mtu anayemuumiza ndugu yake, anayemdhulumu na kumfanyia hiyana, yeye ni adui wa Umoja. (Kwake hauwezi kupatikana umoja, upendo na udugu.) Kama mawazo haya mabaya hayataondoka, Umoja halisi hauwezi kupatikana, ndio maana hatua hii ameiweka kuwa ya kwanza. (Hii ndio faida ya kuwa Jumuiya moja ili umoja na mshikamano uweze kudumu, na hili ndilo kusudio kuu la kuja kwa Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. na ndio makusudio ya Mahdi Aliyeahidiwa ili Waislamu wakusanywe katika mkono mmoja, waweze kuwa umma mmoja.)
Yeye anasema: Muda mwingi inaonekana ya kuwa watu walio wengi wanaposikia maneno kama haya katika vikao kama hivi huathirika moyoni, na wanaliona jambo hili kuwa ni zuri, lakini wanapoondoka katika vikao kama hivi na kuwa pamoja na wenzao marafiki zao hali ile ile mbaya ya zamani inarejea kwao na mambo yale waliyoyasikia wanayasahau, yaani yale mambo mema wanayoyasikia yakisemwa huwa wanayasahau.
(Kwa hiyo mimi ninasema mambo haya yanatakiwa kurudia na kukumbusha kusema mara kwa mara, ili kabla ya kuyasahau tuweze kuyazingatia vizuri.)
Naye anaendelea kusema kuwa tabia ile ile mbaya inaendelea tena kwao, hali hii wanatakiwa kuepukana nayo.
Inabidi kukaa mbali na makundi na vikao ambavyo maneno ya namna hii huzalika na pamoja na hilo inabidi ikumbukwe kwamba mtu lazima ajue vipengele vyote vya mambo mabaya. Kwa sababu ni muhimu sana kwa mtafutaji awe na elimu ya kila kitu. (Yaani kama mtu anatamani au anatafuta kitu fulani basi ni lazima awe na elimu ya kitu hicho kwamba kitu chenyewe kipoje, ni kizuri au kibaya, inatakiwa kuwa na elimu ya vitu vizuri na pia ni lazima kuwa na elimu ya vitu vibaya ili kama ni kibaya akiache na kama ni kizuri basi akichukue).Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s akasema kuwa kama kitu huna elimu nacho (au hukijui) utakipataje? Qurani tukufu imetoa maelezo mara nyingi basi isomeni Qurani tukufu mara kwa mara na mnatakiwa muorodheshe vitendo vibaya na kwa fadhili za Allah na Msaada wake jitahidini kuepukana na mabaya hayo. (Hii ndio hatua ya kwanza ya Taqwa ya kujiepusha na maovu. Ikiwa mtafanya juhudi sahihi basi Allah atawajaalia uwezo wa kujiepusha.) Na mtapewa kinywaji cha kafuri ambacho kitapoza jazba za dhambi zenu. (Kuhusu Kafuri madaktari wanasema ni nzuri sana kupoza Jazba na watu wanaitumia kama dawa pia inatumika na hapa Sayidna Ahmad[as] ameitumia kama mfano katika maradhi ya kiroho yaani kama mtajiepusha na maovu basi hicho ndicho kitakuwa kinywaji cha kaafuri kwa ajili yenu ambacho kwacho taratibu madhambi yenu yatapoa na kuisha.) Baada ya hapo mtajiingiza katika kutenda mema. Maadamu binadamu hatokuwa mcha Mungu basi hatopewa kinywaji hiki na pia ibada zake na dua zake hazitapata rangi ya kukubalika. (kama mnataka kuzikubalisha dua zenu basi kitu cha msingi ni hiki kwamba binadamu aache kufanya maovu na afanye mema na hii ni taqwa ambayo kwa ajili ya kukubaliwa ni sharti muhimu.) Kwani Allah anasema INNAMAA YATAQABALULLAH MINAL MUTAQIIN yaani bila shaka Allah subhana wataala Anawakubalia Wacha Mungu pekee ibada zao. Kwa kweli hata sala na saumu hukubalika za Wachamungu pekee. (Na kukubaliwa kwa ibada hizi nini mradi wake? Akibainisha jambo hili anasema Masih Aliyeahidiwa a.s): Kukubaliwa kwa sala ni huku kwamba baraka na athiri za sala zimeshazalika kwa wanaosali maadamu hizo baraka na athari hazijazalika basi itakuwa ni kazi bure. Sala na saumu ya aina hii ina faida gani kama mtu anasali msikitini na baada ya hapo anaanza kumlalamikia mtu mwingine na kumsengenya. (Watu huuliza tutajuaje kama Allah amekubali sala au ibada ama laa? Basi alama yake ni hii kwamba baada ya sala au baada ya kufanya ibada tunatakiwa tuangalie maovu madogo au makubwa yameshaanza kwenda mbali nasi au la na tumeshaanza kuuchukia au la, ndani yetu tumeshapata hamu ya kutenda mema au la, tumeshaanza kupiga hatua katika kusema kweli au la? Kama jibu ni 'hapana' basi maana yake ibada hii itakua kama kazi bure.) Anasema: Mtu amesali msikitini hapo hapo anaanza kumlalamikia mwingine, kumsengenya, dhana mbaya zinaanza na kuongea maneno yasiyofaa na hiyana imefanywa katika amana. (Kwenye vikao kunakuwa na amana. Na hasa kwa viongozi inabidi wazingatie jambo hili kwamba maneno ya kwenye vikao vya kijamaat yasiongelewe majumbani wala kwa mtu yeyote asiyehusika, jambo hili linatakiwa lizingatiwe, fitina nyingi huzuka kwa sababu hizi kwamba mambo ya amana yanatoka nje. Baadhi ya wakati watu huanza kuwa na husuda na cheo cha mtu fulani na kushambulia heshima ya mtu fulani.)
Masihi Aliyeahidiwa[as] amesema: Kama mtu anajiingiza katika aibu na maovu ya namna hii basi sala imemfaidishaje? (Baadhi ya vijana, mimi ninajua mwenyewe na wengine wanaaniandikia baada ya kuona mambo fulani kwa viongozi au wakubwa wao basi kidogo kidogo huenda mbali na jamaat, kisha wanaanza kwenda mbali na misikiti, kisha wanaenda mbali na ibada hivyo wanakwenda mbali na Allah subhana wataala. Hivyo sala za namna hiyo sio kwamba hazina faida kwa wanaozisali bali pia zinakuwa na hasara kwao. Basi kama tunataka kuvisaidia vizazi vijavyo basi wakubwa na viongozi inabidi wazalishe uchaMungu nafsini mwao.
Akasema hatua ya kwanza kwa yule anayetaka kuwa mumini, ajiepushe na vitendo vibaya na hiyo ndio taqwa. Kisha alisema sehemu nyingine: Kumbukeni kujilinda na vitendo vibaya vilivyodhahiri tu si Taqwa, bali kujiepusha kwa maovu yasiyoonekana ni taqwa, kwa mfano kuhudhuria vikao vya mzaha na upuuzi au kukaa kwenye vikao ambavyo Allah na Mtume wake wanafedheshwa au heshima ya nguduye inavunjwa. Hata asipoafikiana nao lakini ni mbaya sana mbele ya Allah. (Hata asiposhirikiana nao katika mazungumzo lakini kusikiliza mazungumzo yao kwa kukaa nao pia ni mbaya sana mbele ya Allah subhana wataala). Kwa nini alisikiliza mazungumzo haya? Hii ndio kazi ya wale moyoni mwao mna maradhi. Wangejua ubaya kikamilifu wasingefanya hivyo na wasingesikiliza mambo haya kwa kushiriki katika vikao kama hivi. Kumbukeni msikilizaji wa mambo haya ni kama yule anayefanya vitendo hivi vibaya. Waliozungumzia mambo haya wataadhibiwa kidhahiri kwa sababu walifanya dhambi, lakini wale waliokaa kimya watakamatwa pia na kuadhibiwa. Basi kumbukeni sehemu hii kwa umakini sana na kusoma Quran tukufu mara kwa mara na hizi ni amri za Allah zinatakiwa zikumbukwe.
(Basi wale wanaosikiliza mazungumzo mabaya ili wajifurahishe na wanakaa kimya

Endelea uk. 5

Sifa za Waahmadiyya wa Kweli

Kutoka uk. 4

lazima wataulizwa mbele ya Allah. Kisha akaeleza zaidi kwamba muumini hafurahii kwa kuepukana na maovu tu. Tabia hii inapatikana hata katika watu wema wa dini zingine pia na watu wengi duniani huwa wana tabia hiyo kwamba hawafanyi vitendo vibaya.)

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa^{as} akasema: Baadhi ya watu wapo miongoni mwa Mabanyani, Wakristo na dini zingine wasiofanya madhambi kwa mfano baadhi hawasemi uongo, hawanyang'anyi mali ya mwenzao, wanarudisha mikopo badala ya kubaki nayo na wanakua wazuri katika maisha yao ya kila siku. Lakini hili sio jambo Analoridhika nalo Allah. Tunatakiwa kujiepusha na maovu na badala yake kufanya vitendo vizuri bila kufanya hivyo huwezi kupata uokovu. Yule anayejiona kwamba hafanyi dhambi, yeye ni mwehu. Dini tukufu ya Kiislam haimfikishi mtu kwenye daraja la kwanza na kumuacha hapo, bali inataka kukamilisha viwango vyote viwili yaani kuyaacha maovu kikamilifu na kufanya vitendo vizuri kwa ikhlasi. Uokovu hauwezi kuwa mpaka viwango hivi viwili vipatikane.

Anasema: Ninawasihi wanajumuiya tena kwamba songeni mbele katika kumcha Mungu, Yeye pia Atakuwa pamoja nanyi.

Kwa hakika Allah Yu pamoja na wale wanaomcha na kufanya vitendo vyema na hisani. Anasema: Kumbukeni vizuri ikiwa hamtazingatia taqwa na kama hamtafanya matendo mazuri kwa wingi Allah Atawaangamizeni kwanza kwa sababu nyinyi mmekwisha kubali ukweli halafu mnakataa kimatendo. (Yaani mmemkubali Imamu wa zama hizi na kusema kwamba sisi ni bora kuliko Waislamu wengine na tunazingatia wema. Lakini jambo hili litakataliwa kimatendo ikiwa hatutakuwa na Taqwa.) Msilitegemee jambo hili wala msiwe na kiburi kwamba tumejaza bai'ati. Hamtaokoka mpaka mzingatie Taqwa kikamilifu. Allah si jamaa wa mtu yeyote wala Hatampunguzia mtu yeyote. Wapinzani wetu ni viumbe vya Allah nasi pia ni viumbe vyake. Imani tupu haitawasaidia mpaka kauli iendane na vitendo vyenu. (Waislamu wengine pia wana itikadi hiyo kama sisi kwamba Allah ni mmoja na Mtume^{saw} ni Khatamun-nabiyiin na Quran tukufu ni kitabu cha mwisho chenye sheria.) Lakini kama vitendo haviendani na kauli, itikadi na imani kikauli hazitawasaidia. Kimsingi ni vitendo tunavyotakiwa kujitahidi. Kusilimu na kuwa Mwahmadiyya hakutoshi bali ni muhimu kujifanya sawa na maamrisho ya Allah na tuwe waaminio wa kweli Anavyotutarajia Allah.

Kisha Hazrat Masih Aliyeahidiwa^{as} akasema: Allah subhana watalaa Anataka mdhihirishe ukweli kimatendo ili Yeye Awe nanyi. Kama mtakuwa na upungufu katika urehemevu, khulka njema, hisani, vitendo vizuri, ushirikiano au unyenyekevu basi mimi ninajua na mara nyingi nimeshawaambia, jamaat ya aina hii itaangamia. Akasema: Wakati wa Hadhrat Musa^{as} watu wake walipoacha kuzingatia maamrisho ya Allah basi wakaangamizwa kwa radi ijapokuwa Musa^{as} alikuwepo kati yao, mnadhani nyinyi mtasalimika kwa kujaza bai'ati tu?

Kisha Masihi Aliyeahidiwa^{as} akitoa nasaha kuhusu kutanguliza dini juu ya dunia kwa mfano wa Masahaba anasema: Si rahisi kwa mwanadamu kuzalisha hii hali moyoni mwake kwamba atangulize dini juu ya dunia na awe na taqwa. Mfano gani Masahaba walioonesha? Walikuwa tayari kutoa uhai wao katika njia ya Allah. Basi hali hii kuzalika moyoni mwa mtu sio rahisi kuwa awe tayari kutoa uhai wake katika njia ya Allah. Lakini hali ya Masahaba inaonesha kuwa walitimiza wajibu huu. Amri ilipotolewa toeni maisha yenu katika njia hii hawakuigeukia dunia. Kwahiyo ni jambo la muhimu kwamba nyinyi mtangulize dini juu ya dunia. Siku hizi nimekuwa nikitoa hotuba nikielezea maisha ya Masahaba. Tunaweza kukuta matukio ya ajabu sana, walijitolea kwa namna gani? Jinsi gani waliweza kutenda matendo mema? Jinsi gani walikuwa wakizidi katika uchamungu? Viwango vyao vya ibada vilikuwaje? Kwani hawa Masahaba ni mfano mwema kwetu, Mtume^{saw} alisema hivi kuhusu Masahaba:- Masahaba zangu ni kama nyota, yeyote utakayemfuata atakuongoza kwenye njia iliyonyooka. Kwahiyo hawa ni mfano mwema kwetu.

Hazrat Masihi Aliyeahidiwa^{as} akasema: Kumbukeni, yeyote ndani ya jamaat hii akiwa na lengo la kupata dunia basi huyo sio mwanajumuia mbele ya Allah, mwanajumuia hasa mbele ya Allah ni yule tu aliyejitenga na dunia. (Kisha akaeleza) Asidhani yeyote kwamba yeye ataangamia, wazo kama hili ni la kumfanya mtu kuwa mbali na maarifa juu ya Mungu (yaani asidhani hivyo kwamba kama nisipoelekea kwenye dunia nitaangamia). Akasema, anayekuwa mtu halisi wa Allah, Yeye hamuachi kamwe bali Mwenyewe humtosheleza huyo. Allah subhana wataala yupo karibu, mtu yeyote anayezama katika njia ya Allah ndiye hupata mafanikio. Mimi ninasema kwelikweli kwamba Allah Anampenda na kukibariki kizazi cha yule mtu anayetenda sawa na maamrisho ya Allah subhana wataala. Haiwezekani wala haitawezekana kwamba Mungu amuache au aiache iangamie familia ya yule mtu aliyemtii Allah kikweli kweli. Wanaoangamia katika dunia hii ni wale wanaomuacha Mungu na kuiinamia dunia. Je, sio kweli kwamba kila jambo lipo mikononi mwa Allah? Bila yeye jambo lolote haliwezi kupata ushindi, wala maendeleo ya aina yoyote hayawezi kupatikana wala utulivu na raha haviwezi kupatikana. Akasema mali au pesa yaweza kupatikana lakini nani anaweza kusema kuwa baada ya kufa kwake pesa aliyoacha itaweza kuwasaidia mke na watoto? Kuna mifano mingi mbele yetu kwamba baada ya kufariki kwa mtu mali yake pia ikaporwa. Akasema tafakarini sana juu ya mambo haya na fanyeni mabadiliko mapya ndani mwenu. Kisha akasema mpaka sasa jamati ikisifiwa au wanajamati wakisifiwa ni kwa sababu ya Allah subhana wataala ni Mwenye kusitiri lakini pindi mitihani na mabalaa yafikapo yanafichua siri za mtu. Muda huo maradhi yaliyomo moyoni hudhihirika na kuathiri kikamilifu na kumuangamiza mtu.

(Zama zile anazoziongelea Hazrat Masihi Aliyedhiwa^{as} viwango vya uchamungu na amali njema vilikuwa vya juu sana tukilinganisha na zama hizi. Lakini (Hazrat Masihi Aliyeahidiwa a.s) alikuwa na uchungu moyoni mwake. Siku hizi tunaweza kujichunguza wenyewe kwa kuangalia hali zetu. Madai yetu ni yepi na viwango vya amali zetu njema vimekamilika kiasi gani? Akieleza zaidi kuwa mwaminio wa kweli ni nani akasema) Kwa yakini, kumbukeni, mbele ya Allah mwaminio wa kweli ni yule anayetanguliza dini juu ya dunia kama anavyoahidi wakati wa kufanya bai'ati. Kama akitanguliza mambo ya kidunia basi huyo anavunja ahadi ya baiati na kuhesabiwa mkosefu mbele ya Allah.

Akasema, kumbukeni kama hali ya mtu kimatendo haiko vizuri, kukiri kwa ulimi hakuna maana yoyote bali ni matamshi ya bure yasiyo na maana. Imani ya kweli ni ile ambayo inapenya moyoni na kuviboresha vitendo vyake na athari yake. Imani ya kweli ni ya Hazrat Abubakar na maswahaba wengine (Mungu Awaridhie wote) kwani wao walijitolea mali yao na hata maisha yao bila ya kujali chochote. Akasema, siku zote mimi nikifikiria, adhama ya Mtume^{saw} inaathiri moyoni mwangu kwamba watu hao (masahaba) walikuwa wamebarikiwa kiasi gani na athari za kiroho za Mtume^{saw} zilikuwa zenye nguvu gani kwamba aliwafikisha kiwango cha juu? Hebu fikirieni Mtume^{saw} alikowafikisha kutoka wapi. Kuna zama ambapo mambo yote haramu yalikuwa kwao kama maziwa ya mama (yaani walikuwa wakifanya maovu ya kila namna kwa urahisi) walikuwa wakiiba, kunywa pombe, zinaa, ufasiki wa aina zote na dhambi gani ambayo hawakufanya? Lakini kwa sababu ya baraka za kukaa na Mtume^{saw} na malezi yake walipata athari na kubadilika mpaka Mtume^{saw} mwenyewe akatoa ushahidi akisema *Allah Allah fi ashaabi* (yaani unaweza kumpata Allah kuwapitia Maswaba zangu). Masahaba wakavua mavazi ya kibinadamu na kuwa dhihirisho la Allah na hali yao ikawa kama Malaika ambao Yaf'aluna ma yu'marun yaani wanatenda kila walichoamrishwa. Hivyo walivyokuwa maswahaba pia, fikra zao na matamanio ya nafsi yakaondoka kabisa.

Kisha anasema akieleza jinsi gani Mwahmadiyya anatakiwa kuwa baada ya kujaza bai'ati naye anatakiwa kuwa na uhusiano wa aina gani na Jamati, na uhusiano gani na dhati yake (Hazrat Masihi Aliyeahidiwa a.s) katika zama zake, na uhusiano gani na silsila ya Ukhalifa itakayodumu milele baada yake: Tawi lolote lisilokuwa na uhusiano na mti mwishowe linaanguka kwa kukauka. Mtu anayekuwa na imani hai huwa hajali dunia. Dunia inaweza kupatikana kwa namna moja au nyingine. Abarikiwaye ni yule atangulizaye dini juu ya dunia. Lakini atangulizaye dunia juu ya dini ni kama mfu asiyeweza kushuhudia kamwe ushindi wa kweli. Kujaza bai'ati kunaweza kumfaa akitanguliza dini na kujitahidi kuendelea nayo. Bai'ati ni mbegu iliyopandwa ardhini. Kama mkulima yeyote akiridhika na kupanda mbegu tu bila ya kutekeleza faradhi za kupata mazao kama vile bila kupalilia ardhi, kumwagilia maji, kutia mbolea sawa na msimu wala kulinda kama itakiwavyo, anawezaje kutarajia mazao mazuri?

Hudhur akaongeza: Sehemu hii pia ni ya ukulima mwingi na watu wengi hivi karibuni waliotokea Pakistan vijijini kwa kuomba hifadhi kama wakimbizi pia wanajua kwamba shamba lisipotunzwa vizuri baada ya kupanda mbegu mazao hukosekana. Ninataka niwaambie waliokuja hapa hivi karibuni kuwa kwa sababu Allah subhana wataala Amewastawisha hapa kwa kuwapa uhuru wa kufuata dini, wanaweza kutimiza haki ya kufanya ibada, wanaweza kutangaza dini yao kwa hiyo hii ni muhimu sana kwa ajili ya kila Mwahmadiyya hususan waliotoka Pakistan kwamba wajitahidi kutanguliza dini juu ya dunia na wazingatie maamrisho ya Allah subhana wataala kwa uwezo wao wote.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa^{as} anasema: Asiyetunza shamba lake sawasawa, bila shaka litaharibika. Shamba lake litavumilia atakayekuwa mkulima kikamilifu. Hivyo nyinyi pia mmetekeleza aina mojawapo ya kupanda mbegu leo. (Akasema akiwasisitizia waliokuwa mbele yake wakati huo na leo sisi tunatakiwa tusikilize vizuri kwamba sisi pia tumepanda mbegu kwa kukubali Uahmadiyya.) Allah Anajua nani atapata neema gani lakini mwenye bahati ni yule atakayetunza mbegu hii na kufanya maombi kwa ajili ya maendeleo yake. Kwa mfano ilibidi tushuhudie aina mojawapo ya mabadiliko katika kuzingatia sala. Sio hii tu kuwa tumeweza kujenga misikiti. Yatupasa baada ya kujenga misikiti kutimiza haki yake.

Kisha Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa^{as} akatoa nasaha muhimu sana akisema: Zama hizi zimepotea njia sana. Shirk ya aina mbalimbali, bid'ah na maovu mengine zimeibuka. Ahadi ya kutanguliza dini juu ya dunia inayofungwa wakati wa kufanya bai'ati, bila shaka inafungwa mbele ya Allah. Yampasa kila mmoja aizingatie mpaka mwisho wa maisha yake waila itaeleweka hakufanya bai'ati. Ikiwa ataweza kutimiza ahadi hii basi Allah Atatia baraka katika dini na dunia yake. (Hudhur akaongeza: Atatia baraka katika dini na vilevile katika dunia pia.) Zingatieni Uchamungu kikamilifu sawa na matakwa ya Allah. Zama hizi ni nyeti sana. Adhabu ya Allah inashuka. Atakayefanya sawa na matakwa ya Allah atarehemu nafsi yake na watoto wake.

Huzur akasema: Kama alivyosema kwamba adhabu ya Allah inashuka, sisi tunaweza kutazama na tarakimu zinaonesha kwamba matatemeko ya ardhi, tufani na dhoruba zilizotokea katika miaka 100 iliyopita hazikuweza kutokea kabla. Hapa pia mara nyingi tufani inakuja na mvua kubwa pia inanyesha. Kila ikinyesha inasemekana kwamba huu ni mfano wa kipekee katika miaka 500 iliyopita au rekodi ya miongo kadhaa imevunjika. Hii ni nini? Ilibidi tutafakari sisi na kuelewa kwa sababu watu wa dunia hawawezi kuelewa kwamba haya ni maonesho ya hasira ya Allah. Hazrat Masihi Aliyeahidiwa^{as} ameshatoa onyo lililo wazi la mambo haya. Kwa hiyo ilibidi tujirekebishe sisi na kuwaambia watu wengine pia kwamba mabalaa haya sio ya kawaida bali yalitabiriwa kabla ya miaka 100 na njia pekee ya kuepukana nayo ni mtu kumwelekea Mungu tu.

Sasa basi tusiposhika njia hiyo haiyumkiniki kubaki salama. Hivyo mwanadamu mwenyewe amejisababishia matatizo, kama vile vita vinaandaliwa na kudhulumiana kunaendelea. Sawa na mtazamo wetu tunashuhudia kwamba dhulumu imeshazidi kupita kiasi lakini Allah Haadhibu haraka (ili watu wasamehewe). Hata hivyo dhulumu ikizidi kupita kiasi machoni kwa Allah, mwishowe matokeo yake ni haya tu kwamba mataifa yote yadhulumuyo yataangamizwa kwelikweli. Watakaookoka ni wale waliogusiwa katika ubeti huu wa Hazrat Masihi Aliyeahidiwa^{as}:

(tafsiri) ***Kuna moto kwa hakika, ni moto kila mahali,***
watakaookoka na moto huo mkali,
ni wote wapenzi wa Rabbuka,
Mwenye nguvu za ajabu na Jalali.

Basi jambo hili linatakiwa kuzingatiwa sana, nasi tunatakiwa tujitahidi kujiokoa na kuiokoa dunia pia na hatuna budi ila kutumia uwezo wetu wote ili kumpata Allah.

Hazrat Masihi Aliyeahidiwa^{as} anasema: Angalieni, kama mtu asipokula chakula sawa na mahitaji yake hawezi kutosheka vizuri. Je, anaweza kutosheka kwa kupata kipande kidogo tu cha chakula? La hasha. Kama akitia tone moja la maji kooni mwake, hilo haliwezi kumsalimisha na ingawaje amemeza tone moja atakufa kwa kiu. Hawezi kubaki hai mpaka ale au anywe kiasi kinachoweza kuusalimisha uhai wake. (Kuna kipimo maalum cha chakula na maji asipokila aliyeshikwa na njaa na asipokinywa aliyepata kiu, hawezi kusalimika.) Hivyo ni hali ya mtu kujali dini yake. Hawezi kusalimika mpaka hali yake ya kujali dini ifikie kiasi ambacho kinatosheleza kabisa. Tunatakiwa tujali dini, tuzingatie uchamungu na kutii maamrisho ya Allah kama tulavyo chakula na tunywavyo maji mpaka njaa na kiu zinaondoka. Kumbukeni vizuri, kutokutii baadhi ya amri za Allah kunamaanisha kuziacha amri Zake zote. Kama upande mmoja uwe wa Mungu na upande mwingine uwe wa Shetani basi Allah Hapendi kushirikishwa.

Silsila hii (Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya) imeanzishwa kwa lengo hili kwamba mtu aelekee kwa Allah Subhana wataala ingawaje ni viguma sana kuelekea Kwake kwani ni aina mojawapo ya kifo. Lakini mwishoni uhai hupatikana humo. Anayeondoa upande wa kishetani ndani mwake anabarikiwa na baraka zake zinaifikia nyumba yake, nafsi yake na mji wake. Lakini kama akiweza kupata kiasi kidogo tu hatakuwa na baraka. Kujaza bai'ati si kitu chochote mpaka akiri bai'ati kimatendo. Kama ukitamka maneno mengi mbele ya mtu bila ya kutenda chochote, hatafurahi hata kidogo. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo kwa Mungu pia. Yeye ni Mwenye ghera zaidi kuliko wote. Je, inayumkinika upande mmoja mnamtii Yeye, na upande mwingine mnawatii maadui zake pia? Huu ni unafiki. Mja anapaswa asimjali mtu yeyote katika jambo hili na azingatie ahadi yake mpaka mwisho wa maisha yake. (yaani ahadi ya kutanguliza dini juu ya dunia). Uovu una aina mbili. Ya kwanza kumshirikisha Allah, kutokujali ukubwa Wake na kuonesha uvivu katika kumuabudu na ya pili ni kutokuwahurumia viumbe Wake na kutotimiza haki zao. Mnatakiwa msifanye uharibifu wa aina zote mbili, mdumu kwa kumtii Mungu, mbaki na ahadi mliyoifunga wakati wa kujaza bai'ati, msiwaumize waja wa Mungu, msome Qurani Tukufu kwa umakini na kuitekeleza, muepukane na kila aina ya mzaha, mambo maovu na vikao vyenye mambo ya ushirikina, mzingatie sala kwa nyakati zote tano, ilmuradi isiweko amri yoyote ya Mungu mkaipuuza. Safisheni miili yenu na pia takaseni nyoyo zenu na kila aina ya uadui usiojuzu, bughudha na husuda. Mambo haya ndiyo Allah huyataka kwenu. Allah Atujaalie tufanye mabadiliko mema ndani mwetu kwa kutimiza haki za bai'ati. Tukiwa duniani tuweze kutimiza ahadi ya kutanguliza dini juu ya dunia, kutenda matendo sawa na nasaha za Hazrat Masihi Aliyeahidiwaas, na tuelewe maana sahihi ya utii kama ulivyobainishwa katika sharti la kumi ndani ya masharti ya bai'ati na kufikia kiwango chake barabara ili tuwe warithi wa fadhila za Allah Alizoziahidi Hazrat Masihi Aliyeahidiwa^{as}.

Bustani ya Washairi

UJAJI WA MASIHI

Sifa zake mwenye shani, Mola twamuhimidia
Yeye ametuthamini, baraka katuletea
Twamshukuru manani, Mirza katuumbia
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

Kashafika duniani, yeye tulimngojea
Kwa fadhila na hisani, Mirza kumtambua
Kuwa mtu wa thamani, yake kuyafatilia
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

Kasimama ardhini, umoja katuwekea
Kila kona duniani, pembe zote za dunia
Watakuwa mashakani, wale wasomtambua
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

Ameamrisha dini, yake ya mola jalia
Uimara vitabuni, amekwisha fafanua
Katuwekea amani, tusijepotea njia
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

Neno lake lifateni, mbele msijejutia
Pekueni vitabuni, ukweli mtagundua
Kashafika si utani, kuwa wa kufuatilia
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

Alianza Nurudini, baraka alichukua
Walifika hamsini, kwenye kundi hadi mia
Hadi sasa milioni, idadi yaendelea
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

Allah ndio msukani, analotaka amua,
Mohamadi mfateni, elekea yake njia
Wa kukutoa gizani, ni Masihi ndio taa
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

Mwanga huu wenye shani, usiopoteza njia
Sofifia duniani, nuru yake sambazia
Utakuwa hatarini, kamwe sipokuwakia
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

Maneno yenye kifani, yake alotugawia,
Funzo bora shika dini, sala tano ndio njia
Nguzo zote jipakeni, shetani kumuondoa
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

Michango msikitini, uwe mwenye wa kutoa
Wapendeni majirani, kuwa wa kusaidia,
Sadaka kwa masikini, Fungu lao jiwekea
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

Siingie kaburini, silo jambo la sawia
Na subira ishikeni, msiba kikufikia
Majivuno yaacheni, hayo ametuambia
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

Nimefika ukingoni, hapa ninamalizia
Wale mlioamini, kamba moja shikilia
Maombi ndio rubani, pazuri kupafikia
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

Rehema Fadhili
Kitonga, Dar Es Salaam

TUJIUNGE NA Wasiya

Kwa jina Lake Rabuka, Mwenye Rehema karima
Wamadiyya kufunguka, imani pate simama
Siyo wito waa dhihaka, Masihi kapata BIMA
Chonde chende Wamadiyya, Tujiunge na Wasiya

Huzur pata funguka, wazo hilo ni la zama
Limetoka kwa Rabuka, Yule aliye daima
Wengine wahangaika, funuo zapita nyuma
Chonde chende Wamadiyya, Tujiunge na Wasiya

Njia ilo muhafaka, twaitamani daima
Bahato imetufika, duniani na kiyama
Shetani atuzunguka, pande zote hadi nyuma
Chonde chende Wamadiyya, Tujiunge na Wasiya

Tujiunge bila shaka, Mola Atupe kisima
Tupate kuburudika, maishani hadi tama
Matunda yapatikana, waokota walo wema
Chonde chende Wamadiyya, Tujiunge na Wasiya

Kutwa tunahangaika, nyingi mali twazichuma
Twazichuma kama mkeka, nyingi zitakuja kwama
Zakwama bila sadaka, tutoe bila lawama
Chonde chende Wamadiyya, Tujiunge na Wasiya

Wasiya ni muhafaka, maisha yaliyo mema
Tupate kutakasika, baraka ilo daima
Na mali itafurika, ni nyingi shinda mtama
Chonde chende Wamadiyya, tujiunge na Wasiya

Sione wahangaika, Mola atakuoa nema
Subira yahitajika, maombi yake karima
Siku itakubalika, mali isije kukome
Chonde chende Wamadiya, tujiunge na Wasiya

Ahadi isiyoshaka, Masihi akaituma
Molaye akamtaka, hamadiya kujipima
Wasiya sio kutaka, ufunuo ulo uzima
Chonde chende Wamadiya, tujiunge na Wasiya

Zawadi imetufika, tusiende jahanama
Kitabu ameandika, Wasiya ndio salama
Mola aliyetukuka, yote mazuri kasema
Chonde chende Wamadiya, tujiunge na Wasiya

Wala hamtaanguka, dunia hata kiyama
Baraka zitawafika, pamwe na makazi mema
Mtaenda pumzika, mahali palipo nema
Tujiunge wa Wasiya, Wahamadiya kwa wingi

Baridi itawafika, kila mtaposimama
Siku hiyo itafika, tusije laumu nyuma
Wakati usino shaka, tujiunge hima hima
tujiunge na Wasiya, Wahamadiya kwa wingi

Mwanga unatumulika, hatuyajui ya nyuma
Giza limeufunika, mwishowe takuja kwama
Kamba isije katika, tunabudi kupogoma
Tujiunge na Wasiya, Wahamadiya kwa wingi

Ujumbe umeanguka, toka kule kwa mwadhama
Nchini alipofika, kusisitiza ya zama
Sote tuanze funguka, thawabu tupate chuma
Tujiunge na Wasiya, Wahamadiya kwa wingi

Nuruye imechimbuka, vipi tuipige vyuma
Matunda yanang'anika, nasitupate ya chuma
Mtwara ha Nguruka, sote tusikae nyuma
Tujiunge na Wasiya, Wahamadiya kwa mingi

Jambo hili lafanyika, mjue mola katuma
Mjue mola hakika, malipoye kayasema
Pepo itawafunika, duniya hata kiyama
Tujiunge na Wasiya, Wahamadiya kwa wingi

Funuo imetukuka, Huzur apatetuwama
Lilobaki kuamka, tusije kuachwa nyuma
Yeye ndiye mtukuka, mola ampile zama
Tujiunge na Wasyia, Wahamadiya kwa wingi

Na wito umesikika, kule Tanga na Kigoma
Hapana usipofika, kila kona twausoma
Mungu mimina baraka, Nyoyo zipate chegama
Tujiunge na Wasiya, Wahamadiya kwa wingi

Kalamu nninaiweka, akili pate tuwama
Haya yote ni hakika,walahi msiwe nyuma
Msiseme ya dhihaka, yarabi kapata sema
Tujiunge Wasiya, Wahamadiya kwa wingi

Hemedi A Makando, Tanga

MFANO WA KUIGWA:

1. Naanza na Subuhana, muumba Mbingu na Nchi
   Tuwe tunapongezana, mazuri hayajifichi
   Na tusiwe na hiyana, kwenye kuijenga nchi
   Ndugu Tahir Miriza, ni mfano wa kuigwa.
2. Umefanya kazi yako, kama ulivyoambiwa
   Mejitolea kuliko, ulikana kuibiwa
   Uliheshimu miiko, hukutaka kutendewa
   Ndugu Tahir Miriza, ni mfano wa kuigwa.
3. Ulikuwa unakesha, ukisimamia jengo
   Hakuna anaebisha, umehakisi kitengo
   Pia umetukumbusha, kujitoa bila pengo
   Ndugu Tahir Miriza, ni mfano wa kuigwa.
4. Ulikasirishwa sana, wakikosea hesabu
   Uliwaambia Vijana, hukubaki kama bubu
   Hukupenda kulumbana, pia uliwasulubu
   Ndugu Tahir Miriza, ni mfano wa kuigwa.
5. Pia uliwasulubu, wajenge kwa umakini
   Na hukuleta ububu, DEZO wamekuamini
   Wakifunga sukulubu, hawafungi kwa utani
   Ndugu Tahir Miriza, ni mfano wa kuigwa.
6. Umetumwa na Khalifa, kuja hapa Tanzania
   Unastahili sifa, na umefanya kwa nia
   Niige kabla sijafa, thawabu tajipatia
   Ndugu Tahir Miriza, ni mfano wa kuigwa.
7. Ulikosa usingizi, ukuta ukipindishwa
   Haukufanya ajizi, vitu vikibadilishwa
   Mahala hapapendezi, hima palibadilishwa
   Ndugu Tahir Miriza, ni mfano wa kuigwa.
8. Umetufundisha kitu, sisi tuishio hapa
   Haukumtuma mtu, ushirika tulikupa
   Walipoleta vya kutu, na adhabu uliwapa
   Ndugu Tahir Miriza, ni mfano wa kuigwa.
9. Na adhabu uliwapa, wafanyakazi wa DEZO
   Na wala hukuogopa, wakaweka angalizo
   Mola ulimuogopa, ulitii maagizo
   Ndugu Tahir Miriza, ni mfano wa kuigwa.
10. Ulitii maagizo, ukaja Kujitolea
    Haukuwa na vikwazo, juani ulitembea
    Kuziangalia nguzo, je! zimejinyookea?
    Ndugu Tahir Miriza, ni mfano wa kuigwa.
11. Kabla hujaondoka, metupatia zawadi
    Mapenzi ya uhakika, yenye harufu ya udi
    Ni kweli umeondoka, siku nyingine urudi
    Ndugu Tahir Miriza, ni mfano wa kuigwa.
12. Siku ya mwisho kabisa, tuliyapanda Maua
    We mwenyewe hukukosa, ulijua kuchagua
    Ni Maua ya kisasa, hayaungui na jua
    Ndugu Tahir Miriza, ni mfano wa kuigwa.
13. Amesema Subuhana, uislamu usafi
    Si wenyewe tunaona, msikiti ni msafi
    Tutajitahidi sana, kuwa wenye miyo safi
    Ndugu Tahir Miriza, ni mfano wa kuigwa.
14. Ngoja niishie hapa, umefanya mengi sana
    Mwenyezi atakulipa, na thawabu nyingi sana
    Jumuia hii hapa, ina mapenzi mapana
    Ndugu Tahir Miriza, ni mfano wa kuigwa.

Abdallah S. Kalindima
kalindimasenior@gmail.com

MAISHA YA NDOA NI UCHAMUNGU

1. Salamu nawatolea, ndugu zangu wanandoa
   Pongezi nawatolea, safari njema ya ndoa
   Mwenyezi awajalie, maisha mema ya ndoa
   Haya maisha ya ndoa, muushike uchamungu

2. Muushike uchamungu, kizazi kipate njia,
   Baba mama wachamungu,watoto kufata njia
   Mdumu kuomba Mungu, azidi ongoza njia
   Haya maisha ya ndoa, muushike uchamungu

3. Shemeji nakuhusia, husia wangu chukua
   Mumuombe kwa hisia, munyenye pate kukuwa
   Hayo maisha ya ndoa, ukweli nawahusia
   Haya maisha ya ndoa, muushike uchamungu

4. Mshikamane kingie, ukweli nawahusia
   Japo misijaingia, wenzangu nawahusia
   Nami kesho ndaingia, nitaukuta husia
   Haya maisha ya ndoa, muushike uchamungu

5. Ndoa nusu ya dini, tuliamo kiingia
   Mshikamane kidini,shetani sijeingia
   Atawatoa kundini, maovu kuyazingia
   Haya maisha ya ndoa,muushike uchamungu

6. Ujumbe namalizia, majivuno kimbizia
   Tabia njema kazia, moyowe uwe pazia
   Shikamana na jamii, Ile ilokuzunguka
   Haya maisha ya ndoa, muushike uchamungu

7. Ndoa ni jambo la kheri, wanandoa tutambue
   Mmeingia kwa heri, mshikamane hebue
   Wanandoa kwa herini, ibada dumu dawam
   Haya maisha ya ndoa, muushike uchamungu

Madumla Ng'amilo, Tuangoma
Dar es salaam

Kisa cha Mvulana Kipofu

Mvulana mmoja aliye kipofu alikuwa amekaa kwenye ngazi za jengo moja na kofia yake ameitandika miguuni kwake. Alishikilia bango lililosema: "Mimi kipofu jamani, saidia tafadhali." Palikuwa na sarafu chache tu kwenye kofia yake ile aliyoitandika.



Mtu mmoja aliyeonekana akitembea akiharakisha karibu na jengo alimuona yule mvulana. Yule mtu akasimama, akafikiria kwa muda. Akatoa sarafu chache toka kwenye mfuko wake na kuzidondosha kwenye ile kofia. Kisha akalichukua lile bango, akaligeuza, na akaandika maandishi fulani juu yake. Akalirudisha lile bago katika namna ambayo kila mmoja aliyepita njia aliweza kuyaona yale maneno mapya.



Punde ile kofia ikaanza kuchangiwa haraka haraka. Watu wengi zaidi walikuwa wakimpa fedha yule mvulana kipofu.

Mchana ule yule mtu aliyebadilisha lile bango alikuja kuona namna mambo yanavyokwenda. Mvulana akazitambua hatua za nyendo zake na akauliza, "Wewe ndiye yule uliyebadilisha bango langu asubuhi hii? Uliandika nini?" Yule mtu akasema, "Niliandika ukweli tu. Nilisema ulichokisema wewe lakini katika njia tofauti."



Alichokiandika kilikuwa:

"Leo ni siku ya kupendeza na siwezi kuiona"

. . . . . .

Tafakuri:

Unafikiri bango la kwanza na la pili yalikuwa yanasema kitu sawa?

Bila shaka mabango yote yaliwaambia watu kuwa mvulana alikuwa kipofu. Lakini bango la kwanza lilisema tu yu kipofu. Bango la pili liliwakumbusha watu kwamba wamebarikiwa sana ya kwamba wao si vipofu.

Na Yeye ndiye Aliyewaumbieni masikio na macho na mioyo: ni kidogo mnayoyashukuru. (Sura Al-Mu'minun; aya ya 78)

CHEMSHA BONGO



KWENDA KULIA

4 Chuo cha Ubashiri
6 Alichaguliwa kuwa Khalifa 1982
8 Mhamiaji
11 Jina la Makao makuu
12 Mkutano wa mwaka
13 Mwakilishi baada ya Mtume

KWENDA CHINI

1 Mwongoza sala
2 Asiye na dini
3 Maana yake ni kujitupa kwa Allah
5 Msamaha
6 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
7 Mwezi wa kumi katika kalenda ya kiislam
9 Ujumbe toka kwa Allah
10 Sambaza

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno yafuatayo kwa kuyazungushia na Penseli

UFUNUO	TAASISI	DISEMBA	ZAGAZA
KALAM	ELEKTRONIKI	MSAADA	SAMBAZA
MAJNUNI	NGUVU	WASIA	SOGA
TABLIGH	BIBLIA	UKWELI	TAKWIMU
TEHAMA	YESU	MASIHI	ZIARA
SAFAA	ARDHI	ATHARI	
MARWA	FADHILA	UHALIFU	
SADR	NASAHA	MWANYA	

W	A	S	I	A	G	T	F	T	I	N	I	A	I	Y
T	M	A	R	W	A	B	A	H	I	K	A	H	D	U
A	B	H	G	M	W	D	D	T	I	F	I	G	M	K
K	T	G	B	M	A	R	N	N	A	S	T	A	K	W
W	A	K	L	A	A	J	O	S	A	Y	Z	A	C	E
I	B	T	S	Q	K	R	N	M	B	A	M	O	R	L
M	L	M	Z	N	T	R	G	U	B	R	U	G	M	I
U	I	K	T	K	A	L	A	M	N	N	M	A	W	D
Y	G	B	E	S	V	S	A	U	U	I	R	T	A	I
E	H	L	I	Y	O	S	A	F	H	A	F	A	N	S
S	E	W	N	B	Z	G	U	H	I	A	P	A	Y	E
U	K	M	L	V	L	S	A	Z	A	D	L	S	A	M
N	G	U	V	U	G	I	A	T	H	A	R	I	H	B
L	F	A	D	H	I	L	A	D	K	B	N	S	F	A
W	X	Z	A	G	A	Z	A	Y	R	H	G	I	F	U

Mapitio ya Hotuba za Jalsa Salana 2018

Inatoka uk. 12

kiroho na imani itakuwa wazi zaidi kuliko hapo kabla. Satelaiti kwa sasa inasaidia sana urushaji wa matangazo na bishara hii inatimizwa kupitia urushwaji wa MTA. Takwimu zinaonyesha kwamba watumiaji wa intaneti pekee wakiwa takriban milioni 23 kwa sasa ambao ni wastani wa asilimia 50 ya Watanzania wote kwa sasa. Katika kilele cha mafanikio hayo cha TEHAMA Jamaat Ahmadiyya Tanzania tuna kiwanda cha uchapaji kwa ajili ya kuchapisha vitabu, magazeti, majarida na vipeperushi mbalimbali. Tuna gazeti la Mapenzi ya Mungu, Redio Ahmadiyya 99.3 FM Mtwara na MTA Tanzania Studios katika kufikisha ujjumbe wa Allah katika kila kona ya nchi yetu. Aidha, tuna akaunti mbalimbali za mitandao ya kijamii kama vile Twitter, Facebook, Youtube, na tovuti yetu www.ahmadiyyatz.org.

Hivi leo tunashuhudia pia jinsi Allah anavyozidi kufungua mianya na njia mpya za kuzagaza ujumbe wake kupitia mitandao ya kijamii. Katika dunia ya sasa yafahamika wazi ya kwamba baadhi ya watu wanakosa muda kabisa kuangalia luninga na hivyo kulazimika kufuatilia habari, matukio au mikutano kupitia mitandao ya kijamii na wavuti kwa kutumia vifaa vya kieletroniki kama vile kompyuta, vifaa vya mkononi. Tovuti ya www.alislam.org inafanya kazi saa 24 ikiwa na hazina kubwa ya elimu ya jamaat kupitia video na machapisho mbalimbali kama vitabu, magazeti, majarida na makala mbalimbali. Wanafunzi walioko shuleni na vyuoni na watumiaji wote wa mitandao kwa ujumla wanaweza kujipatia baraka nyingi kwa kuitumia vyema tovuti hii kujielimisha mambo mbalimbali ya Jamaat na Islam kwa ujumla.

TEHAMA ina changamoto zake hivyo ni vyema kujiuliza je tunaweza kuishi kulingana na mafundisho ya Islam katika zama hizi za maendeleo ya TEHAMA? Tukumbuke Allah Anasema: "***Leo nimewakamilishieni dini yenu, na kuwatimizieni neema Yangu, na Nimewapendeleeni Islam iwe dini yenu***"(5:4). Akifafanua aya hii Khalifatul Masih II Hadhrat Mirza Mahmood Ahmad*ra* alisema "ujumbe umekamilika ukiambatana na baraka za kiwango cha juu kabisa ambacho mwanadamu anaweza kupata kutoka kwa Allah. Ujumbe huu umebebwa na neno Islam ambayo maana yake hasa ni kujitupa kwa Allah. Allah Ametukamilishia dini yetu na Kuitimiza neema yake kwetu na kuifanya Islam kuwa dini yetu hivyo muongozo umekamilika. Hivi sasa tunaweza kuishi katika zama zozote ziwazo kwa kutumia muongozo wa Islam."

Kuhusiana na kukumbatia au kushikamana na mafundisho ya Islam Allah mwenyewe Anasema "***Na shikeni kamba ya Allah nyote, wala msiachane***" (3:104). Kwa ujumla kuna vitu vitatu, ambavyo ni Qur'an Tukufu, Mitume wa Allah na Makhalifa wa Allah.

Qur'an Tukufu ni neema ya Allah ambayo Ameitimiza juu yetu, ni chemchem ya baraka zisizo kikomo kwa wanadamu. Na kuhusu Mitume wa Allah, Allah Anasema kumhusu Mtukufu Mtume*saw* "***bila shaka mnao mfano mwema katika Mtume wa Allah...***"(33:32). Tena Allah Anasema "***Sema: Ikiwa ninyi mwampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni, Mwenyezi Mungu Atawapendeni na Atawaghofirieni madhambi yenu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye ghofira, Mwenye rehema***" (3:32). Kwa hakika kila apendaye kuwa na maungano na Allah ni faradhi kwake kuwa na maungano na Mtukufu Mtume Muhammad Mustafa*saw*. Seyidna Ahmad*as* alisema Baada ya mapenzi ya Allah, Nimelevywa na mapenzi ya Mtukufu Mtume Muhammad Mustafa*saw*, kama huu ni ukafiri basi mimi ni kafiri namba moja.

Kama ilivyoshuhudiwa siku zilizopita, wakati wa Mtukufu Mtume Muhammad*saw*.

Mapinduzi makubwa ambayo aliyaleta kufuatia kudhihiri kwake yalikadiriwa na Allah yaendelee na kuimarika kupitia mfumo wa Ukhalifa.

Hakika sote ni mashuhuda wa maendeleo makubwa yanayofikiwa na Jumuiyya hii kila kukicha kupitia Kamba hii ya Ukhalifa.

Iwe katika zama hizi za maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano au maendeleo mengine yoyote yawayo au yatakayokuja katika uso wa dunia, Basi jibu lake ni hili tu ya kwamba tushikamane barabara na Ukhalifa wa Kiahmadiyya.

Katika zama hizi za maendeleo ya sayansi na Teknolojia kwa ujumla hatuna njia nyingine yoyote ya kukabiliana na jambo lolote linalokuja mbele yetu hata kama liwe dogo kiasi hiki lifanane na chembe ya haridari, isipokuwa kwa kushikamana na Ukhalifa.

Ukhalifa ni roho yetu, uhai wetu, uzima na maisha yetu. Ukhalifa ni nuru pekee inayotufikisha kwa Mtukufu Mtume Muhammad*saw* na kwa Mwenyezi Mungu.

Ikiwa tunataka kushikamana na Mafundisho ya Islam katika zama hizi basi tushikamane na Ukhalifa kwa kumuombea sana Hadhrat Mirza Masroor Ahmad, Khalifatul Masih V*atba*, Allah ampe nguvu, afya na umri mrefu katika kuihudumia Islam na wanadamu, Tudumishe maungano yetu kwa kumuandikia barua katika mambo yetu ya kiroho na kidunia Na daima tudumu kuangalia hotuba zake za ijumaa na vipindi vyake vingine kupitia MTA, Kupitia Ukhalifa tutapata muongozo wa kila jambo.

Pamoja na faida za teknolojia hii pia zipo athari mbaya kama matumizi sahihi hayatazingatiwa. Kwa bahati mbaya sana, Rika la vijana ni wahanga wakubwa katika athari hizi.

Vijana hutumia muda mwingi kwenye mtandao na kompyuta, Wanalevywa na intaneti kiasi cha kushindwa kuzingatia Muda, Sala, Usomaji wa Qurani na majukumu mengine wawapo mtandaoni. Hii huwafanya wawe mbali na Allah.

Khalifa Mtukufu V*atba* mara kwa mara amekuwa akituonya kuhusu hatari za intaneti, kompyuta, simu na vifaa vingine vya kielektroniki.

Kwa mfano, Katika mkutano wa mwaka (Jalsa Salana) wa Uingereza mwaka huu, Huzur*atba* alitahadharisha namna simu zinavyoweza kutenganisha familia na kuchochea vitendo viovu kwa rika la vijana.

Ni vema kuwa na uangalizi wa karibu kwa watoto na vijana wetu katika matumizi ya vifaa vya kielektroniki ili kuhakikisha matumizi sahihi na ya kiasi yanazingatiwa.

Pia tujiweke mbali vitu visivyoruhusiwa kama vile kupoteza muda, kupiga soga, kutoheshimiana baina ya wadogo na wakubwa na Kuchanganyikana wanaume na wanawake (kutokuzingatia hijabu).

Kwa ujumla dunia haiko salama dhidi ya Teknolojia hii, kutokana na kukosekana kwa usiri na usalama, Matumizi ya muda mwingi katika mitandao na intaneti, Picha na video zisizo na maadili, Matangazo mabaya kama vile matangazo ya pombe, sigara, kamari, mashindano ya urembo n.k,

Kuingilia Mawasiliano ya mtu bila ridhaa yake, Mwingiliano wa mawasiliano, Viharibu taarifa (virusi), Uhalifu wa mtandaoni kama vile shambulizi la kimtandao na ugaidi wa kimtandao, na unyanyasaji wa kimtandao hususani kwa wasichana.

Kwa mujibu wa ripoti ya takwimu za jinai ya mwaka 2014 iliyotolewa na tume ya taifa ya takwimu kwa kushirikiana na jeshi la polisi inataja uhalifu wa kimtandao kama moja ya makosa ya jinai yanayochipukia kwa kasi na kuhatarisha usalama wa watumiaji wa mitandao na teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa ujumla hapa nchini.

Ripoti hiyo inataja uhalifu wa mitandao kuwa ni pamoja na Uhalifu wa kutumia Kompyuta, Simu na vifaa vingine vya kielektroniki ambavyo vinauwezo wa kuhifadhi taarifa katika mfumo wa mtandao wa kompyuta.

Kesi za uhalifu wa mtandao 380 zilizoripotiwa mwaka 2014 ikiwa ni ongezeko la asilimia 14 toka kesi 333 za mwaka 2013.

Hii inaashirikia kukua kwa tatizo hili hapa nchini, Hivyo kama waminio ni vema kuchukua tahadhari.

Athari za makosa ya uhalifu wa mtandao zinzotajwa na ripoti hiyo ni pamoja na

Kuathiri uchumi wa taifa, Mmomonyoko wa maadili, Upotevu wa mali na fedha na uharibifu wa miundo mbinu mbalimbali.

Tunapoangazia matumizi sahihi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ni vema pia kufahamu na kuzingatia sheria mbalimbali zihusika na udhibiti wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano hapa nchini, ili kujilinda na kujiepusha dhidi ya hatia za matumizi mabaya ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano sawa na sheria za nchi.

Ninamuomba Allah Atuwezeshe sote kushikama barabara na Ukhalifa wa kiahmadiyya, kukubali, kupokea na kujifunza Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na kuitumia vizuri kwa ajili ya Malezi na Mahubiri. Amin.

Kila Sifa Njema inamstahiki Allah, Mola wa Ulimwengu.

Siku ya Michezo Yanogeshwa Jamia Ahmadiyya





Jamia Ahmadiyya,Morogoro

Kwa fadhila za Allah taasisi nyeti ya Jamia Ahmadiyya nchini imeendelea kupata maboresho na mafanikio mapya siku hadi siku.

Hii ni katika kutumia ahadi za Allah Alizomwahidi Hadhrat Masih-il-Mau`uud[as] juu ya mafanikio ya jumuia yake na taasisi zote zilizomo ndani yake. Katika kusherehekea siku ya michezo, iliyofanyika tarehe 31/10 hadi tarehe 1/11/2018 taswira mpya nzuri na ya kuvutia ilionekana-yaani baadhi ya michezo mipya hapa kwetu iliongezeka.

Siku ya michezo ilifunguliwa rasmi tarehe 31/10/2018 saa 1:30 asubuhi kwa usomaji wa Quran Tukufu iliyosomwa na AL-USTAADHI RAMADHANI ABBAS MKIETI na kufuatiwa na nasaha chache kutoka kwa mgeni rasmi aidha Mkuu wa Chuo alisema pamoja na kuwa haya ni mashindano ambapo



ndani yake kunakuwa na ushindani, lakini wasisahau suala zima la kuhurumiana na kupendana(fair play). Baada ya hayo Mkuu wa Chuo aliongoza maombi ya kimya na kupiga mpira kuashiria kuanza kwa mashindano.

Siku hiyo mchezo wa kwanza ulikuwa ni mpira wa wavu(volley ball) uliozikutanisha timu za 'Amaanat' na 'Shujaat',ambapo timu ya Shujaat iliibuka na ushindi wa seti 2-0.

Baada ya mchezo huo, lilifuata shindano la kuvuta kamba. Katika shindano hilo lilikutanisha tena timu za Amaanat na Shujaat safari hii timu ya Amaanat iliibuka na ushindi.

Kisha likafuata shindano la kuruka(long jump),hili ni shindano la mtu mmoja mmoja na matokeo ni kwamba mshindi wa kwanza ni Muhammad Mussa Nyamawi na wa pili ni Ridhwan Ibrahim.

Baada ya hapo lilifuata shindano la kukimbia kwa miguu matatu,hili ni shindano la watu wawili wawili. Katika shindano hili, washindi wa kwanza walikuwa ni Muhammad Mustapha na Rajab Ibrahim wa pili walikuwa ni Qassim Kimwaga na Twahir Bilal.

Baada ya shindano hilo lilifuata shindano la riadha mita 100 kwa wanafunzi wa darasa la hifidhi na mshindi wa kwanza alikuwa ni Abdulrahman Ramadhan, wa pili Twahir Said.

Kisha likafuata shindano la kukimbia miguu matatu kwa wanafunzi wa hifidhi ambapo washindi washindi wa kwanza walikuwa ni Shadad Said na Ally Hajji na wa pili walikuwa ni Shaban Abdallah na Kamran .M. Ahmad.

Baada ya hapo lilifuata shindano la kulenga shabaha kwa kutumia manati ambapo mshindi wa kwanza alikuwa ni Muhammad .M. Nyamawi na wa pili alikuwa ni Rajabu Luseza.

Shindano lililofuata baada ya hilo ni kusukumana kwa kusimamia mguu mmoja(thabit Qadami),katika shindano hili mshindi ni Idrissa Juma na wa pili ni Mahmood Diega.

Kisha likafuata shindano la mpira wa meza(table tennis) ambapo mshindi alikuwa ni Shaban Yunus na wa pili ni Shadad Said.

Shindano la kusukumana kwa kusimamia mguu mmoja (thabit Qadami) kwa wanfunzi wa hifidhi mshindi wa kwanza ni Abdulrahman Ramadhan na wa pili ni Nadhir Ramadhan.

MASHINDANO YA WATUMISHI WA JAMIA (MASHEKH NA WAALIM)

Mashekh na waalim pia hawakubaki nyuma siku hiyo ya michezo,kwani nao walishiliki katika michezo mbalimbali kama vile; kukalia kiti ambapo mshindi wa kwanza katika shindano hili alikuwa ni Shekh



Hafeedh sahib na wa pili ni Shekh Aziz .A. Shahzad sahib.

Shindano lingine kwa upande wa watumishi lilikuwa ni kujaza maji kwenye chupa kwa kutumia mikono,Ndoo ya maji inawekwa kwa umbali wa mita 3.

Mshindi wa kwanza katika shindano hili alikuwa mwalimu Abadallah Ramadhan sahib na wa pili ni mwalimu Athuman Takato sahib.

KIVUTIO KIKUU

Kivutio kikubwa katika siku za michezo ni mchezo wa mpira wa miguu ambao ulizikutanisha timu za Shafqat na Shuja'at ambapo mpaka dakika 90 za mchezo zinakamilika timu ya Shuja'at iliibuka na ushindi wa bao 1-0.

Mchezo mwingine uliovuta hisia na hamasa kubwa kabisa miongoni mwa watazamaji ni mchezo wa kuruka vihunzi na vizuizi mbalimbali.

Katika mchezo huu,washiriki walipewa ujumbe ambao walitakiwa waufikishe mwisho wa shindano baada ya kupita katika vizuizi vingi vikiwemo kutembea kwa kutumia matofali ya madongo ya kuchoma na kupita kwenye bwawa lililojaa matope nk.

Kwa ujumla siku ya michezo mwaka huu ilifana sana –Alhamdulillaah.

Tukio la Kusisimua Tabligh za Miamvuli

Tukio moja la kufurahisha limetokea huko Banana Ukonga katika mahubiri yanayoendeshwa na Ansarullah Ilaqa ya Dar es salaam. Mnamo tarehe 27-11-2018 kundi la mabinti wa sekondari lilikuwa limesimama kati yao alipata nafasi ya kukaa karibu kabisa na meza yetu. Binti aliyekaa aliwaomba wenzie wamuokotee kipeperushi kilichokuwa mtaroni (kimetupwa) wanafunzi watatu kati yao walikataa na mmoja (wa kati ya kundi hilo) aliingia mtaroni na kukiokota huku muombaji akiulizwa swali kuwa umekionaje wakati kimo mtaroni? Akajibu kuwa nimekijua kwa sababu kwanza nilipewa na mimi nikaombwa kabla sijakisoma. Baada ya kupewa kipeperushi hicho (Uislam Hauna Uadui na Ukristo) alikifuta vumbi kwa kitambaa chake na kukinyoosha mikunjo mikunjo hadi kikapendeza na kuanza kukisoma.

Nilifurahishwa sana kwa namna alivyokishughulikia hadi kuanza kukisoma. Hivyo nilipata wazo la kumzawadia gazeti la *Mapenzi ya Mungu* kwa busara aliyoonyesha mbele ya wenzake. Hatimaye wanafunzi wawili mmoja aliyeingia mtaroni na mmoja kati ya wale waliokataa kuingia mtaroni walimvamia mwenye gazeti kila mmoja alishikilia gazeti kwa kulitaka. Hapo gazeti likawa katikati ya mikono mitatu na hatimaye kwa busara yake akaruhusu gazeti lichukuliwe na binti aliyeingia mtaroni ili kulinusuru lisichanike kwa sharti la kusoma na kumrudishia.

Inafurahisha na ni mfano mzuri kwa kulinda machapisho yetu.

MATUKIO KATIKA PICHA



Matembezi ya amani kuadhimisha siku ya uhuru yaliyoandaliwa na Majlis Khuddamul Ahmadiyya tarehe 1 Disemba 2018.



Khuddamul Ahmadiyya pamoja na Sadr Ansarullah wakifanya usafi Hospitali ya Taifa Muhimbili baada ya matembezi ya kuadhimisha uhuru mnamo Disemba Mosi 2018.



Amir na Mbashiri Mkuu akihutubia wanajumuiya wa Iringa kwenye mkutano



Khuddamul Ahmadiyya tayari kwa kufanya usafi Hospitali ya Taifa Muhimbili baada ya matembezi ya kuadhimisha uhuru mnamo Disemba Mosi 2018.



Amir na Mbashiri Mkuu (kulia) na Sheikh wa Mkoa wa Iringa (kushoto) wakiweka jiwe la msingi la msikiti huko Iringa



Wanajamaa wa Iringa wakisikiliza mada za mkutano kwa makini



Amir na Mbashiri Mkuu na Wajumbe wa Majlis Amila Taifa pamoja wanajumuiya wakiwa uwanja wa ndege na Mkaguzi wa Mahesabu toka Markaz Mirza Mahmood Ahmad siku ya kuondoka kwake baada ya siku 13 za kazi hiyo nchini



Amir na Mbashiri Mkuu na Wajumbe wa Majlis Amila Taifa pamoja wanajumuiya katika picha ya pamoja na Mkaguzi wa Mahesabu toka Markaz Mirza Mahmood Ahmad siku ya kuondoka kwake baada ya siku 13 za kazi hiyo nchini

Ziara ya Ansarullah Mikoani Yafana

Na **Ally Khamis Mbambwa**
Sadr Ansarullah

Ash-haduAllaailahaillallah, Wa Ash-hadu Anna Muhammadan 'Abduhuu warasuuluh.



Wawakilishi wa Ansarullah Morogoro

Mimi ninaahidi kwa dhati kwamba, nitajitahidi kujitolea maisha yangu yote, kusambaza na kulinda Ahmadiyya katika Islam. Na nitasimama imara katika kulinda na kutetea Ukhalifa. Sitasita kujitolea chochote kwa ajili hii.
Zaidi ya hayo nitajitolea kuhakikisha watoto wangu wamejitolea na kutumika kwa ajili ya Ukhalifa wakati wote. Inshallah.



Ansarullah wa Kituo cha Newala

Hicho ni kiapo kilichoongozwa na Sadr Ansarullah katika ufunguzi wa vikao mbalimbali alivyoviendesha katika ziara yake aliyoifanya katika baadhi ya mikoa hapa nchini.

Ziara ilianza tarehe 08/08 hadi tarehe 18 katika mikoa ya Kagera(Katoma na Kagenyi), Mwanza, Mara (Tarime),Tabora, Singida, Dodoma na Morogoro.

Hali kadhalika ziara hiyo iliendelea Tarehe 22 hadi 28 Oktoba 2018 katika mikoa ya Lindi na Mtwara ambapo palikuwa na vituo sita Wana Ansarullah kutoka matawi mbalimbali walikusanyika. Vituo vikuu vilikuwa ni Kilanjelanje, Mtama, Newala, Masasi, Nachingwea na Mtwara Mjini

Katika ziara hizo, Sadr Sahib aliambatana na wajumbe wa Majlis Amila Mulk ya Tanzim ya Ansarullah - Tanzania Mzee Hemed Sheikh Ubwa, Bw. Mwinyimvua Ussi, Mwl Hamidii Kaigwa na Bw. Karim Mpate.

MALENGO YA ZIARA HIYO

1. Kuangalia utekelezaji na Utendji wa majukumu ya Ansarullah katika ngazi za Mikoa na matawi yake.
2. Kuangalia utekelezaji wa ajenda za shura za mwaka huu 2018 ambazo ni:-
   i. Ansarullah Wajitolee zaidi kufanya Mahubiri
   ii. Ansarullah wajiimarishe katika Malezi
   iii. Utekelezaji wa ajenda ya Bajeti
   iv. Mchango wa Jengo la ofisi za Ansarullah
3. Maagizo kutoka Kwa Khalifa Mtukufu kuwa:-
   i. Viongozi wote wa Tanzim ya Ansarullah wajiunge na nidham ya Wasia.
   ii. Ansarullah wasikilize hotuba za Khalifa Mtukufu na kuangalia vipindi vya MTA n.k

Maagizo mengine yalikuwa ni:-
- Utumaji wa taarifa za mambo yaliyotekelezwa katika matawi ni jambo lilotiliwa mkazo.
- Kuwakumbusha Ansarullah wote kushiriki Ijtmaa ya Kitaifa itakayofanyika 14 hadi 16 Disemba 2018 Kitonga Dar es Salaam.

Mwezi Disemba 2018 utakuwa ni mwezi wa uchaguzi wa kuchagua Mazaim wa matawi.

Hakika ziara ilikuwa ni nzuri na yenye mafanikio makubwa. Pamoja na kuangalia utekelezaji wa majukumu mbalimbali, Sadr Ansarullah Bw. Ally Khamis Mbambwa alikabidhi Meza na Miamvuli katika matawi kadhaa kwa ajili ya kuanzisha vituo vya kudumu vya Mahubiri.


Ansarullah wa Tabora

Pia madarasa ya Malezi yalifanyika kwa kuwasilishwa mada mbalimbali juu ya kukumbushana wajibu wetu katika utekelezaji wa majukumu yetu kama kusimamisha Sala tano tena kwa jamaa, Mahubiri, Kujitolea, kuwahudumia viumbe wa Allah n.k. pia

Tunamuomba Allah Ajalie ziara hizi zilete uimara katika utekelezaji wa Majukumu yetu kwa ajili ya Tanzim ya Ansarullah,



Ansarullah wa Kagenyi Kagera

Jamaat Ahmadiyya na Islam kwa ujumla.

Umrah (Hija Ndogo) - Sehemu ya Pili

Na **Ali R. Mohammed - Safarini Qatar**
Kutoka toleo Lililopita

2. **Daarul Arqaam**

Kutoka kule Daarun Nad'wa, tunarudi tena ndani ya Masjid Haraam.

Tungeweza kutumia *King Abdul Aziz Gate* lakini tutumie *Baabu Salaam Gate* lengo sio kutoka nje tena, tunaishia ndani ya hii Corridor ya Safaa na Marwa tukiendelea kumtukuza Allah kwa unyeyekevu na Sauti za chini tukiondozana nao kuelekea kilima cha Safaa... Lakini safari yetu sisi inaishia hapa pembezoni kabla ya kufika mwisho wa Corridor hii.

Hapa hakuna Alama yoyote zaidi ya Taa hii hapa chini kubwa...



Mahala hapa ndipo Nuru ya Islam ilipoanzia. Na ndipo palipoanza kuondoa huzuni na Upweke aliojihisi kuwa nao Mtume^{saw} mwanzoni kabisa alipoanza kazi ya Allah ya kuihubiri na kuifundisha Islam.

Hii sasa ni DAARUL ARQAAM.

Hapa ni nyumbani kwa Bwana Arqam bin Abu Arqam^{ra} ambapo Mtume Muhammad^{saw} akiwa na watu wachache sana mwanzoni kabisa waliojiunga na Islam walikuwa wakijifunza dini ya Islam kwa siri katika nyumba hii.

Bwana Huyu na Bibi Khadija Umul Mu'miniin^{ra} ndiyo waliokuwa wakiwaalika jamaa na marafiki kwa Siri katika nyumba hii wafike kujifunza dini ambayo ndo mwanzo Mtume^{saw} anaanza kufundisha huku mke wa bwana huyu akiandaa chakula kwa ajili ya wageni na hivyo katika nyumba iliyosimama mahala hapa ndipo palipopandwa Mbegu ya Islam.

Nyumba hiyo ambayo iliitambulika pia kwa Jina la Daarul Khaizaran ina mambo mengi ya kusisimua katika Islam, licha ya dini kuanza kufundishwa hapa kwa Siri, na mengine mengi cha kuvutia zaid ni kisa cha kusisimua pale utakaposikia ya kuwa Khalifa wa pili wa Mtume^{saw} Seydna Umar bin Khataab^{ra} kuwa alisilimu katika nyumba iliyokuwa mahala hapa ambapo alifika na upanga wake kwa lengo la kumuua Mtume Mtukufu^{saw}.

3. **Kilima cha Abu Kubay**

Sasa tuendelee mbele katika katika Corridor hii ya Saa'i (Inayotumiwa kukimbia Baina ya Safaa na Mar'wa) kuelekea kilima cha Safaa.

Tasbihi, dhikri nyingi kwa Allah Mola Muumba zinaendelea.

Hapa tunazunguka eneo la Saa'i na kurudi kushoto Sawa kuifuata Corridor kama kawaida kuelekea tena Mar'wa. Baada ya Mita kadhaa, sisi hatuelekei tena Mar'wa. Macho yetu ni upande wetu wa kuume kuitafuta Baab Salaam na tunatoka nje kabisa ya Masjid Haraam kwa mlango huu wa Salaam.

Tunapoangaza mbele upande wa kuume kidogo Macho yetu yanakutana na nyumba zilizo juu ya kilima. Japo kilima hiki kimekuwa kikivunjwa katika Shughuli mbalimbali za upanuzi wa Masjid Haraam, lakini kilima kidogo kama alama bado kipo.

Katika Kilima hiki - Jabal Abu Kubay ndipo mahala ambapo kwa mara ya Kwanza palifanyika mkutano wa Kwanza wa Hadhara


Picha ya kilima cha Abu Kubay

wa Mtume Muhammad^{saw} kuwahubiria watu wa Makka, huku Hadhara hiyo ikiandaliwa na Wazee na Wakuu wa makabila makuu ya Watu wa Makka bila wao kutambua kwambua kwamba ule ndo ulikuwa ndiyo ufunguo wa Nuru ya Allah Kwao.

Hapa aliombwa ishara ya ukweli wa madai yake ndipo aliponyooshea kidole chake katika mwezi na ukaonekana umepasuka vipande viwili.

Watu kadhaa walikubali kusilimu wakati huo, lakini bado wazee na wakazi wengine walikataa na kusema kwamba huu ni Uchawi dhahiri.

4. **Mahala alipozaliwa Mtume Muhammad^{saw}**

Itaendelea toleo lijalo

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

RAB. I - RAB. II 1439 AH | NOVEMBA 2018 | FATAH 1397 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abdullah bin 'Amr bin 'Aas r.a. ya kuwa Mtume s.a.w. alisema: Mwislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wanasalimika katika ulimi wake na mkono wake na Muhajir (Mhamaji) ndiye yule ayahamaye Aliyoyakataza Mwenyezi Mungu. (Bukhari)

Mapitio ya Hotuba za Jalsa Salana 2018

Na Mwandishi Wetu

MAFUNDISHO YA ISLAM KATIKA DUNIA YA TEHAMA

Baada ya kumshukuru Allah na kumtakia rehema Mtume mtukufu^{saw} Sadr Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania Ramadhan Hassan Nauja sahib alimshukuru Amir sahib kwa kumkabidhi na kumuamini juu ya jukumu la kutoa mada hiyo.

Alisema ya kwamba; itakumbukwa katika Jalsa Salana ya kimataifa iliyomalizika hivi karibuni jijini London Uingereza Khalifa wetu mpendwa Hadhrat Mirza Masroor Ahmad^{atba} alieleza kwa marefu na mapana pamoja na kutoa miongozo kadhaa kuhusiana na malezi ya watoto na mwenendo wa wanajumuiya kwa ujumla katika matumizi ya Teknolojia ya habari na teknolojia. Alianza hotuba yake. Teknolojia ya habari na mawasiliano au TEHAMA kwa kifupi hurejea mifumo yote ya kieletroniki inayotumika katika kutengeneza, kuhifadhi, kuchakata na kutumia habari kiatika mifumo tofauti tofauti kama vile picha, n.k. TEHAMA inahusika na matumoizi ya kompyuta, wavuti, satelaiti, picha, matangazo ya redio na luninga na mambo mengine mengi yanayofanana na hayo. TEHAMA inaendelea kukua kila siku, alisema Sadr sahib.

Allah Mjuzi wa Ghaibu Alitoa utabiri wa mabadiliko haya miaka elfu moja na mia nne iliyopita kama anavyosema katika Qur'an Tukufu "***Siku Tutakapoikunja mbingu kama mkunjo wa karatasi za maandiko: kama Tulivyoanza umbo la awali Tutalirudisha tena; ni ahadi iliyo juu Yetu; bila shaka Sisi ni Wafanyao***" (21:105). Khalifatul Masih II Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad^{ra} akifafanua aya hii anasema; Allah Alikusudia kuumba mbingu na ardhi mpya (Islam) wakati wa Mtume Mtukufu Muhammad^{saw}, ambapo mbingu na ardhi za kale zitaangamizwa. Kama Allah Anavyoashiria Akisema; ***Siku Tutakapoikunja mbingu kama mkunjo wa karatasi za maandiko...***"(21:105). Maendeleo ya upagani na ustaarabu wa magharibi ukafunika mbingu na ardhi mpya iliyoundwa na Mtukufu Muhammad^{saw} kwa muda, Allah Akaahidi kuirejesha mbingu na ardhi ile kupitia juhudi za mfuasi wa Mtukufu Muhammad^{saw} Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi, kama Allah Alivyosema "***...kama Tulivyoanza umbo la awali Tutalirudisha tena...***" (21:105).

Aliendelea kunuu aya ya sura ya 81:8 "Na nafsi zitakapounganishwa" ambapo alisema aya hii inabashiri wakati wa maendeleo wa njia za usafiri na mawasiliano zitarahisishwa sana kiasi kwamba watu wa mataifa mbalimbali watakusanywa pamoja. Uvumbuzi wa treni, ndege, magari na maendeleo ya TEHAMA ikijumlisha kompyuta, simu, satelaiti, intaneti, mitandao ya kijamii, redio, viwanda vya uchapaji, n.k. vimetajwa katika aya hii tena Allah Akisema "***Na sahifa zitakapoenezwa***"(81:11)

Kuhusu maendeleo ya sayansi ya anga na uvumbuzi wa satelaiti Allah pia anasema "***Na utando wa mbingu utakapotanduliwa***" (81:12). Hadhrat Mirza Mahmood Ahmad^{ra} anasema wakati wa Masihi Aliyeahidiwaas sayansi ya anga itakuwa kwa kasi kiasi cha kuishangaza dunia na kuashiria katika zama hizi milango ya sayansi na elimu za

Endelea uk. 8

Ifahamu Majlis Ansar Sultanul Qalam



Na Issa Salum Disowile - Katibu MASQ

Sultanul Qalam ('Mfalme wa kalamu") ni jina lenye nguvu kubwa alilopewa Masihi Aliyeahidiwa^{as} kupitia ufunuo. Masihi Aliyeahidiwa^{as} anasema: "Allah ameniita mnyenyekevu Sultan Al Qalam, '*mfalme wa kalamu*' na ameita kalamu yangu Zulfiqar Ali au upanga wa Ali" (Al-Hakam, Jal. V, No. 22, Uk. 2).

Ni ufunuo huo tu ambao ulihamasisha kuanzishwa kwa Majlis Ansar Sultanul Qalam ("Wasaidizi wa Mfalme wa Kalam").

Masihi Aliyeahidiwa^{as} anaandika kwamba "kuna amani kila mahali; ni kwa kutumia kalam tu Islam hushambuliwa. Na hii ndio sababu kwamba lazima kalam itumike kujibu mashambulizi hayo." (Malfoozat, Jal. 8, Uk. 20) Kauli hii ya Masihi Aliyeahidiwa^{as} inaonyesha kazi ambayo kalam inafanya katika siku hizi au zama hizi.

Majlis Ansar Sultanul Qalam (MASQ) ilianzishwa na Hadhrat Musleh Mauud^{ra} mwaka 1922. Lengo kuu la MASQ ni kulinda na kueneza mafundisho sahihi ya dini tukufu ya Islam.

Katika mwaka 2011, Hadhrat Khalifatul-Masih V^{atba} alikumbushia juu ya umuhimu wa MASQ aliposema, "….Kipindi hiki haitoshi tu kwamba Waahmadiyya 200 au 300 wajiunge na Majlis Ansar Sultanul Qalam, na kuingia katika uwanja huu wa mahubiri (Tabligh). Badala yake Khuddamul Ahmadiyya wote wahusike katika hili, siku zote ikumbukwe kwamba kanuni ya Allah ni kuishi pamoja na kutendeana kwa wema"(Ijtmaa ya Majlis Khuddamul Ahmadiyya – Ujerumani, 2011).

MASQ imeanzishwa chini ya Mjlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania. Na Khuddam kutoka pande zote nchini wanatakiwa kujiunga na kundi hili na kuweza kushiriki moja kwa moja katika Jihadi hii ya kalamu, kwa kujibu tuhuma mbali mbali dhidi ya Islam kupitia magazeti, Makala, mitandao na hata barua, ili kueneza mafundisho sahihi ya Islam.

Ni muhimu kwa kila mmoja wetu kufahamu chimbuko la Majlis Ansar Sultanul Qalam (MASQ), lengo lake, na haja ya sisi kuingia katika mpango huu wenye baraka na kusimama kuutetea Uislam katika zama hizi. Ni wito kwa Khuddam wote kuanza kazi mara moja, lazima tusimame na kujibu tuhuma zinazotolewa dhidi ya Islam na Jama'at ya Imam wa zama, kwa kutumia ufahamu wetu na weledi wa hali ya juu. Hii ni safari ambayo si tu kwamba tunaihudumia Islam bali tunajihudumia sisi wenyewe ambao tunavuna faida nyingi kadri ufahamu wetu unavyokua.

Hivyo ni wito kwa kila Khuddam na Atfal kuitikia wito huu wa mpendwa wetu Huzur^{atba} na kujiunga katika idara hii iliyobarikiwa duniani. Mwenyezi Mungu anasema: "(Naapa kwa) kidau na kalamu na yale wayaandikayo, kwa neema ya Mola wako wewe si majnuni" (Al-Qalam: 2-3).